JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU NGAZI YA CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2022

## MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU NGAZI YA CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2022

# 614 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI .. 2

2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Nchi yetu Tanzania ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Nchi yetu Tanzania ........ 6
2.1.3 Swali la 3: Sayari Dunia ........ 9
2.1.4 Swali la 4: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo ........ 12
2.1.5 Swali la 5: Nchi yetu Tanzania ........ 14
2.1.6 Swali la 6: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika ........ 17
2.1.7 Swali la 7: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika ........ 20
2.1.8 Swali la 8: Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo ........ 24
2.1.9 Swali la 9: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru ........ 27
2.1.10 Swali la 10: Ushirikiano wa Kimataifa ........ 31
2.2 Sehemu B: Maswali ya Insha ........ 33
2.2.1 Swali la 11: Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika ........ 34
2.2.2 Swali la 12: Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo ........ 38
2.2.3 Swali la 13: Dunia Sayari ........ 44
2.2.4 Swali la 14: Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo ........ 50

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........ 56

4.0 HITIMISHO ........ 57

5.0 MAPENDEKEZO ........ 57

KIAMBATISHO ........ 58

## DIBAJI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Ualimu Daraja A uliofanyika Mei 2022 kwa masomo ya Jiografia na Historia ambayo hutahiniwa kwa pamoja katika mtihani wa Maarifa ya Jamii. Lengo la kuandaa taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa, watunga sera, wakufunzi, walimu tarajali na wadau wengine wa elimu. Mitihani ni namna mojawapo ya kufanya tathmini ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Tathmini hiyo inawezesha kubainisha ufanisi, changamoto pamoja na kutoa mapendekezo kuhusu mwelekeo wa namna bora ya kutekeleza mtaala wa ngazi husika.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali za mtihani wa Maarifa ya Jamii ulikuwa mzuri. Kati ya mada saba zilizotahiniwa, ufaulu ulikuwa mzuri katika mada sita na mada moja ilikuwa na ufaulu wa wastani. Aidha uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa uliofanyika umebaini kuwa, kwa ujumla, ufaulu katika mtihani huo ulikuwa mzuri kwani asilimia 99.97 ya watahiniwa walifaulu. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, sababu za watahiniwa kufaulu kwa kiwango kizuri katika mada mbalimbali ni kuwa na maarifa ya kutosha pamoja na kuzingatia matakwa ya maswali. Uchambuzi wa kina na sababu za ufaulu katika kila swali umebainishwa.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, uchambuzi uliobainishwa kwenye taarifa hii utasaidia katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia na hivyo kuinua ufaulu wa watahiniwa katika Mitihani kwa wakati ujao. Uchambuzi huu utasaidia wakufunzi pamoja na walimu tarajali kufanyia kazi dosari zilizobainika na kuendeleza namna bora ya ufundishaji na ujifunza na hivyo kuwa na walimu bora wa somo la Maarifa ya Jamii katika shule za msingi.

Baraza linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika maandalizi ya taarifa hii.



Athumani S. Amasi
KATIBU MTENDAJI

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inahusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa mtihani Ualimu wa somo la Maarifa ya Jamii kwa ngazi ya cheti Daraja la A (GATCE) uliofanyika mwezi Mei 2022. Maswali ya mtihani yalitungwa kwa kuzingatia Mihtasari ya mwaka 2009 ya masomo ya Jiografia na Historia kwa ngazi ya cheti Elimu ya Msingi na fomati ya Mtihani wa Maarifa ya Jamii ya mwaka 2022.

Mtihani wa Maarifa ya Jamii uligawanyika katika sehemu mbili (A na B) zenye jumla ya maswali kumi na nne. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi kati ya hayo, maswali saba (7) yalipima taaluma na matatu (3) yalipima utaalamu wa ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama nne (4). Hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 40. Sehemu B ilikuwa na jumla ya maswali manne (4) ya insha ambapo maswali mawili (2) yalipima taaluma na mawili (2) yalipima utaalamu wa ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15, hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60. Kwa hiyo, katika mtihani wa Maarifa ya Jamii, mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne.

Katika kufanya uchambuzi, ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika makundi matatu. Mfiko wa asilimia za ufaulu katika makundi hayo ni 0 – 39, 40 – 69 na 70 – 100 mtawalia. Ufaulu wa watahiniwa umeoneshwa kwa kutumia takwimu, jedwali na chati ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu. Sababu za watahiniwa kuwa na ufaulu hafifu, wastani au mzuri zimebainishwa. Ili kufafanua hoja zilizotolewa kuelezea sababu za majibu ya watahiniwa, sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika kama vielelezo ili kuonesha namna watahiniwa walivyoweza au kushindwa kujibu swali lililochambuliwa.

Uchambuzi kuhusu ufaulu wa jumla katika mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 3,273 walisajiliwa kufanya mtihani huo. Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 3,266 sawa na asilimia 99.97 walifaulu kwa daraja A hadi D. Watahiniwa saba sawa na asilimia 0.03 walipata daraja F. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umepanda kwa asilimia 0.14 ikilinganishwa na ufaulu wa watahiniwa katika somo hilo mwaka 2021, ambapo asilimia 99.83 ya watahiniwa walifaulu.


## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ilikuwa ya maswali mafupi. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii. Hivyo, watahiniwa wote 3,273 walifanya maswali hayo. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama 4. Kwa ajili ya kufanya uchambuzi na tathmini, ufaulu wa watahiniwa katika kila swali uligawanywa katika makundi matatu; ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri. Mfiko wa alama katika kila kundi ulikuwa 0 - 1.5, 2 - 2.5 na 3 - 4 mtawalia.

#### 2.1.1 Swali la 1: Nchi yetu Tanzania

Swali la kwanza lilitoka katika mada ya Nchi yetu Tanzania. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kuelezea kwa kifupi ni kwa namna gani mwinuko kutoka usawa wa bahari, mikondo ya bahari, latitudo na umbali wa eneo kutoka usawa wa bahari hufanya maeneo kuwa na tabianchi zinazotofautiana. Takwimu zinaonesha kuwa, ufaulu katika swali hilo ulikuwa hafifu kwani ni asilimia 82.8 ya watahiniwa walipata ufaulu wa alama 0 hadi 1.5. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 1.





**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 1*

Kama takwimu zinavyoonesha katika Chati Na. 1, asilimia 82.8 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu hafifu. Asilimia 10.0 ya watahiniwa wengine walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi

2.5, na asilimia 7.2 tu ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3.0 hadi 4.0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa uliofanyika katika skripti zao ulibaini kuwa asilimia 82.8 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Watahiniwa hao, walishindwa kubaini ni kwa namna gani mwinuko, umbali kutoka usawa wa bahari, mikondo ya bahari na latitudo husababisha tofauti ya tabianchi kati ya eneo moja na lingine katika uso wa Dunia. Watahiniwa wengi katika kundi hili, walieleza sababu za kutokea kwa mambo tajwa kama tabianchi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *mvutano wa kani mbalimbali unaotokea ndani ya Dunia huweza kusababisha mwinuko na mikondo ya bahari kuweza kutokea katika uso wa Dunia.* Mtahiniwa alieleza jambo linalosababisha kutokea kwa mwinuko na mikondo ya bahari, ingawa kimsingi alitakiwa aeleze ni namna gani mwinuko kutoka usawa wa bahari na mikondo ya bahari vinavyosababisha tabianchi kutofautiana. Aidha, baadhi ya watahiniwa walieleza jinsi majanga ya asili na shughuli za binadamu zinavyoathiri tabianchi katika baadhi ya maeneo. Wengine waliorodhesha aina za tabianchi bila kutoa maelezo yoyote.

Kwa ujumla, watahiniwa hawa walipaswa kueleza kuwa tabianchi inamaanisha jumla ya halijoto, unyevuanga, kani eneo ya anga hewa, upepo, usimbishaji na tabia nyingine zinazoathiri hali ya hewa ya sehemu fulani ya uso wa Dunia kwa muda fulani (miaka 30). Hivyo watahiniwa katika kundi hii walipaswa kuonesha ni kwa namna gani tabianchi inavyoathiriwa na mwinuko na umbali kutoka usawa wa bahari, mikondo ya bahari na latitudo. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa kwa swali hili.


1 i) Mwinuko Kutoka usawa wa bahari, huathiri tabia ya nghi kwa Kuonesha hali tofauti tofauti za hewa.

ii) Mikondo ya bahari. Mikondo hii hutofautiana Kwasababu sio Katika maeneo yote Kuna bahari na hutofautiana Kulingana na muelekeo.

iii) Latitudo. Hii pia husababisha tofauti Katika baadhi ya maeneo Kwasababu latitudo hutofautia na hivyo Kila eneo lina latitudo yake.

iv) Umbali wa eneo Kutoka baharini, hutofautiana Kutokana na mawio na machweo yatakayo tokea Katika eneo kwa siku.

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 1.


Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alitoa majibu yaliyo kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, katika kipengele cha (ii) alieleza mikondo ya bahari kutofautiana kulingana na uelekeo, badala ya kutaja aina za mikondo (mkondo joto na baridi), na kueleza jinsi inavyoathiri tabianchi ya eneo husika.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani ambao ni asilimia 10.0, wengi wao waliweza kubaini matakwa ya maswali. Wengi wa watahiniwa katika kundi hili walikuwa na uelewa wa wastani kwa swali hili. Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa kutoka kwenye skripti zao unaonesha kuwa watahiniwa wengi katika kundi hili walipata alama za wastani kwa sababu baadhi yao walieleza hoja chache tofauti na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa wengine walieleza hoja zote nne ingawa baadhi ya hoja hizo zilikuwa siyo sahihi, jambo lililosababisha washindwe kupata alama zote. Kwa ujumla, majibu ya watahiniwa katika kundi hilo yalionesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo yanayosababisha utofauti wa tabianchi kati ya eneo moja na lingine.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri ambao ni asilimia 7.2 katika swali hilo walieleza athari za mwinuko, umbali kutoka usawa wa bahari na mikondo bahari katika kusababisha tofauti ya tabianchi kati ya eneo moja na lingine kwenye uso wa Dunia. Watahiniwa hao waliweza kueleza kuwa kadiri mwinuko unavyoongezeka kwa mita 100 kutoka usawa wa bahari, ndivyo kiwango cha joto hupungua kwa nyuzi 0.6 $^{0}$C. Hii inamaanisha kuwa

maeneo yaliyoinuka kama mlima Kilimanjaro huwa kuna baridi kali na mvua nyingi kileleni ikilinganishwa na maeneo yaliyo pwani na sehemu tambarare.

Aidha, watahiniwa katika kundi hili pia walieleza jinsi mikondo ya bahari inavyoathiri tabianchi ya eneo husika. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa hawa walieleza kuwa sehemu inayopitiwa na mkondo bahari joto mara nyingi huwa na mvua za kutosha wakati sehemu inayopitiwa na mkondo bahari baridi huwa na ukame au hali ya jangwa. Pia, watahiniwa walibainisha jinsi latitudo zinavyoathiri tabianchi kwa kueleza kuwa maeneo maeneo yaliyo karibu na mstari wa Ikweta huwa yana hali joto ya juu kuliko yaliyo mbali na mstari wa Ikweta ambayo huwa na baridi. Vilevile, walieleza kuwa maeneo yaliyo jirani na Ikweta hupata mvua nyingi ukilinganisha na yale yaliyo mbali na Ikweta. Kwa upande mwingine, watahiniwa hao walieleza kuwa umbali kutoka baharini huathiri kiasi cha joto katika sehemu husika kwa kuwa hupoza pepo mwanana za bahari. Aidha, maeneo mengi ya pwani hupata mvua nyingi ikilinganishwa na maeneo yaliyo mbali na ukanda wa pwani. Kielelezo Na.1.2 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika kundi hili.


(i) Mwinuko kutoka usawa wa bahari ⇒ hutofautisha tabia ya nchi kwa kuwa kila unavyozidi kupanda au kuinuka nyuzi joto hupungua kwa kiwango cha 0.6°C kutoka katika usawa wa bahari.

(ii) Mikondo ya bahari ⇒ pia mikondo ya bahari huwe za kutofautisha tabia ya nchi kwa sababu mikondo ni tofauti kuna mkondo wenye joto na mkondo wa bahari wenye baridi.

(iii) Latitude ~~na umbali~~ ⇒ pia hutofautisha kwa sababu maeneo yaliyo karibu na Ikweta hupata joto zaidi kuliko yale yaliyo mbali na ikweta.


(iv) Umbali wa eneo kutoka baharini ⇒ watu walio karibu na bahari hupata joto sana kuliko walio mbali na bahari.

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 2.

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha jibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa aliyeweza kueleza jinsi tabianchi inavyoweza kuathiriwa na mwinuko kutoka usawa wa bahari, mikondo ya bahari, longitudo na latitudo pamoja na umbali kutoka baharini.

### 2.1.2 Swali la 2: Nchi yetu Tanzania

Swali la pili lilitoka katika mada ya Nchi yetu Tanzania. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi namna matukio mbalimbali ya asili yanavyoweza kumsababishia binadamu majanga. Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 69.8 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walipata ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa.





**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 2*

Kama takwimu zinavyoonesha katika Chati Na. 2, asilimia 69.8 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4. Asilimia 18.2 ya watahiniwa wengine walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi 2.5, na watahiniwa asilimia 12.0 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa uliofanyika katika skripti zao ulibaini kuwa watahiniwa asilimia 69.8 waliokuwa na ufaulu mzuri walieleza matukio mbalimbali ya kiasili na namna yanavyoweza kumsababishia binadamu majanga. Watahiniwa hao walieleza matukio ya kiasili na kutoa mifano halisi ya matukio yanayosababisha maafa na kuleta uharibifu wa mali za binadamu na miundombinu. Katika majibu yao, wengi wa watahiniwa hao walieleza jinsi matukio ya asili kama vile mvua nyingi, mfano mvua ya el-nino iliyotokea Tanzania mwaka 1998, ukame uliotokea mkoa wa Arusha na Manyara mwaka 2006 na Kaskazini Mashariki mwa Kenya mwaka 2003 na 2004, yalivyosababisha vifo vya watu na mifugo. Pia, watahiniwa hao walieleza jinsi matetemeko ya ardhi pamoja na milipuko ya volcano inavyoweza kusababisha vifo, uharibifu wa mali na miundombinu. Wengi wa watahiniwa katika kundi hii waliweza kutaja

tetemeko la ardhi lilitokea mkoani Kagera mwaka 2016 kama mfano katika majibu yao.

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika kundi hii ulibaini pia kuwa watahiniwa walikuwa na dhana sahihi kuhusu matukio mbalimbali na madhara yake kwa binadamu. Kwani baadhi ya watahiniwa walibainisha kuwa ili tukio lionekane kuwa ni janga ni lazima lihusishe uharibifu wa mali za watu na vifo na litokee katika hali ya kushutukiza na katika eneo kubwa la kijiografia. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


2
- Tetemeko la ardhi. Hii huweza kusababisha
uharibifu wa majengo pia husababisha kifo
kwa binadamu.

- Mafuriko. Pia Mafuriko huweza kusababisha
madhara makubwa mfano kuharibu mazao
shambani, pia hata vifo kwa binadamu na wa
nyama.
- Mlipuko wa Volkano. Ni janga hili huweza
kusababisha vifo kwa watu ambao wanaki
a karibu na milima hiyo
- Kimbunga. Janga jingine ni kimbunga amba
cho huharibu mazingira, huharibu uoto
na pia kuharibu makazi ya watu.


Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi kwa swali la 2.

Katika kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa katika hoja zake aliweza kueleza matukio mbalimbali ya kiasili yanayoweza kumsababishia binadamu majanga.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha washindwe kupata ufaulu mzuri katika swali hilo. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walieleza hoja kwa kuirudia ili ionekane kama ni hoja mbili tofauti, na watahiniwa wengine walitoa maelezo machache ambayo hayakujitosheleza ili waweze kupata alama kamili. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja chache tofauti na matakwa ya swali. Katika hatua nyingine, baadhi ya watahiniwa walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yao. Kwa mfano, miongoni mwa majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa ni kama vile: *kuzalishwa kwa virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO (CORONA) katika maabara, kupanda kwa bei za mafuta na vyakula duniani kutokana na vita vya Russia*

*na Ukraine na ongezeko kubwa la watu Duniani*. Majibu haya hayakuwa sahihi na yalitolewa na baadhi watahiniwa ambao walishindwa kutofautisha kati ya majanga ya asili na majanga ya kibinadamu. Pia, wapo watahiniwa waliotaja matukio ya kiasili kama vile: *tetemeko la ardhi, mafuriko, ukame* na *jangwa* bila maelezo yoyote. Kutaja matukio ya kiasili bila kutoa maelezo yoyote ni kiashiria kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa mdogo au hawakujua matakwa ya swali.

Watahiniwa asilimia 12.0 waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa kuhusu matukio ya kiasili na athari yake kwa maisha ya binadamu, mali na miundombinu. Wengi wa watahiniwa hao walieleza matukio ya kibinadamu na madhara yake kama matukio ya kiasili. Wengine walieleza jinsi shughuli mbalimbali za binadamu kama vile *uwindaji, uchimbaji wa madini, uvuvi haramu, ukataji miti ovyo, uchongaji wa vifaa hatarishi* na *ulaji mbaya wa baadhi ya vyakula* vinavyosababisha majanga kwa binadamu. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa hao walieleza jinsi *uchimbaji wa madini unavyosababisha mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa vyanzo vya maji, makazi ya binadamu na viumbe hai.* Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


2

(i) Uwindaji ni matukio ya kihistoria ambayo mtu huweza kuwinda polini na kunyatwa na nyoka

(ii) Kula nyama mbichi hupelekea mtu kupata magonjwa ya tumbo

(iii) Kutumia vifaa kama vile kisu huweza kusababisha magonjwa


(iv) Uchongaji wa vifaa kwa kutumia moto hii huweza kusababisha mtu kuungua

Kielelezo Na. 2.2. Sampuli ya jibu lisilo kwa swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2, majibu ya mtahiniwa yalikuwa na dosari katika hoja zake na hivyo kupata alama hafifu. Mtahiniwa huyo alieleza matukio ya kibinadamu na madhara yake kama matukio ya kiasili kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.3 Swali la 3: Sayari Dunia

Swali la 3 lilitungwa kutoka katika mada ya Sayari Dunia. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza umuhimu wa kuelewa dhana ya mistari ya Ikweta, Kansa, Kaprikoni na Griniwichi katika maisha ya binadamu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa wa mzuri kwa kuwa asilimia 70.3 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 2 hadi 4, kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 3.





**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 3*

Takwimu katika Chati Na. 3 zinaonesha kuwa asilimia 40.1 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 30.2 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 29.7 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa uliofanyika katika skripti zao ulionesha kuwa, asilimia 40.1 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo walieleza umuhimu wa kila mstari kwa kuainisha matukio na tabianchi kwa mistari ya latitudo na longitudo. Watahiniwa hao walieleza jinsi mstari wa Ikweta unavyoigawa Dunia katika sehemu kuu mbili za kizio cha Kaskazini na kizio cha Kusini. Pia, walibainisha umuhimu wake katika kupungua kwa joto na mabadiliko ya tabianchi kadri unavyoelekea Kusini au Kaskazini mwa ncha za Dunia. Baadhi yao walieleza kuwa karibu na Ikweta usiku na mchana huwa ni masaa 12 tofauti Kaskazini na Kusini mwa ncha ya Dunia. Watahiniwa walieleza kuwa mstari wa Griniwichi ni mstari unaochorwa kwenye ramani kutoka ncha ya Kaskazini hadi Kusini mwa Dunia katika sehemu kuu mbili Mashariki na Magharibi. Mstari huu kwa jina lingine huitwa meridiani na hutumika katika kukokotoa muda. Aidha, watahiniwa hao walielezea umuhimu wa mstari wa Tropiki ya Kansa

kwenye mabadiliko ya tabianchi. Watahiniwa hao walieleza kuwa mstari wa Tropiki ya Kansa upo nyuzi $23^{1}/_{2}$ Kaskazini mwa Ikweta. Wakati wa jua la utosi, eneo la kizio cha Kaskazini huwa na ongezeko la joto, baridi hupungua na mvua hunyesha wakati huo. Aidha, kwa upande wa mstari wa Tropiki ya Kaprikoni, watahiniwa hao walieleza kuwa upo nyuzi $23^{1}/_{2}$ Kusini mwa Ikweta. Wakati wa jua la utosi, eneo la kizio cha Kusini huwa na ongezeko la joto, baridi hupungua na mvua hunyesha wakati huo.

Majibu ya watahiniwa hao yalionesha kuwa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mistari ya latitudo na longitudo, hivyo waliweza kupata alama za juu. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


3 (i) Ikweta; Ni mstari ambao unaugawa dunia kati ka vizio viwili. watu wanao kuwa karibu na ikweta wanapata mvua nyingi
(ii) Greenwich; Ni mstari ambao unaugawa dunia katika sehemu mbili yaani sehemu ya kulia na sehemu ya kushoto.
Huu ndo mstari wa ikweta
Huu ndo mstari wa Greenwich
(iii) Tropiki ya kansa; Ni kizio cha kaskazini ambacho kinaonesha nyuzi 23½ kati kizio chake.
(iv) Tropiki ya kaprikoni; Ni kizio cha kusini ambacho kinaonyesha nyuzi 23½


Kielelezo Na.3.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1, hoja za mtahiniwa zilieleza kwa ufasaha umuhimu wa dhana ya mistari ya Ikweta, Kansa, Kaprikoni na Griniwichi katika maisha ya binadamu. Mtahiniwa alieleza mistari hiyo inapatikana wapi na umuhimu wake. Japo hoja zake zilikuwa na dosari kidogo kwa mfano katika hoja ya (i) kuhusu mstari wa Ikweta, mtahiniwa hakueleza vizio viwili ni vipi yaani hakutaja Kaskazini na Kusini. Pia, katika mstari wa Griniwichi, hakueleza kuwa hutumika kukokotoa muda katika Dunia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa mistari mbalimbali inayochorwa kwenye ramani ya Dunia. Baadhi ya watahiniwa hao, walishindwa kutofautisha majina, au kutambua umuhimu wa mistari hiyo katika maisha ya binadamu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

*mstari wa kansa huwa na nyuzi* $23^{1}/_{2}$ *kusini mwa Ikweta* na *mstari wa kaprikoni huwa na nyuzi* $23^{1}/_{2}$ *kaskazini mwa Ikweta.* Jibu kama hili ni mojawapo ya majibu yanayoashiria kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majina, umuhimu na mahali mistari husika ilipo katika ramani ya Dunia.

Asilimia 29.7 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu. Watahiniwa hawa hawakuwa na ufahamu kuhusu umuhimu wa mistari inayochorwa kwenye ramani. Katika kundi hilo, baadhi ya watahiniwa waliandika hoja zihusuzo kupatwa kwa Jua na Mwezi, matetemeko ya ardhi, kupwa na kujaa kwa maji, majira ya mwaka, umbali kati ya Dunia na Jua, kupanda na kushuka kwa bei za mazao katika soko la Dunia. Aidha, baadhi ya watahiniwa walieleza jinsi mistari hiyo inavyosaidia katika utengenezaji wa barabara, uimarishaji kilimo cha mazao ya biashara, na upimaji wa kiwango cha joto cha mahali fulani. Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kuwa, hawakuwa na ufahamu kuhusu umuhimu wa mistari mbalimbali itumikayo katika ramani ya Dunia, sababu zinazosababisha kupwa na kujaa kwa maji, kupanda na kushuka kwa bei za mazao katika soko la Dunia, na vipimo mbali mbali vitumikavyo kupima hali ya hewa. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi kwa swali la 3.





Kielelzo Na.3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 3.

Jibu la mtahiniwa katika kielelezo Na. 3.2 siyo sahihi kwa kuwa, badala ya mtahiniwa kueleza umuhimu wa kila mstari wa Longitudo na Latitudo, mtahiniwa ameorodhesha mistari hiyo bila kutoa maelezo. Hivyo, kuorodhesha haikutosha kumpa alama kwani mistari hiyo ilikwishatajwa katika swali.

### 2.1.4 Swali la 4: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo

Swali la nne lilitungwa kutoka katika mada ya Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Jiografia. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kuunga mkono kwa ufupi kwa kutoa hoja nne juu ya kauli ya kuwa, "Upimaji na tathimini ni kitu muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia'. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 87.5 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 4, kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 4.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 87.5 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 11.0 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi 2.5, na asilimia 1.5 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika skripti zao ulionesha kuwa, asilimia 87.5 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo waliweza kutoa hoja zilizothibitisha kauli ya kuwa "upimaji na tathimini ni kitu muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia". Watahiniwa hao walitoa hoja kama vile; *humwezesha mwalimu kutunza kumbukumbu za alama za maendeleo ya wanafunzi katika somo la Jiografia*; *humwezesha mwalimu kutambua uwezo wa wanafunzi kabla ya kuanza ufundishaji mada fulani, au baada ya kufundisha mada husika katika somo la Jigrafia*. Aidha, watahiniwa hao waliongeza kuwa upimaji na tathimini *humwezesha mwalimu kutambua uwezo wa wanafunzi kabla ya*

*kuanza kufundisha stadi za kijiografia, kujua uelewa wa wanafunzi katika mada mahsusi* na *kubaini tofauti za uelewa wa somo kati ya wanafunzi*.

Aidha, watahiniwa walieleza umuhimu wa upimaji na tathmini katika kutoa ushauri kwa uongozi wa shule na kwa wazazi. Hii ni kama vile ufuatiliaji wa maendeleo ya wanafunzi na namna ya kuwaandaa wanafunzi. Kwa mfano mtahiniwa aliandika kuwa; *upimaji husaidia kubaini wanafunzi wenye mahitaji maalum*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.



4 i/ Upimaji na tathmini humsaidia mwalimu kuboresha njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji.
ii/ Upimaji na tathmini humsaidia mwalimu kubaini changamoto za wanafunzi na kuweza kuzitatua
iii/ Upimaji na tathmini humsaidia mwalimu kujua mwanafunzi ameelewa kwa kiasi gani na kufanya uamuzi sahihi.
iv/ Upimaji na tathmini humsaidia mwanafunzi kuwa na ari ya kujifunza


Kielelezo Na.4.1. Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alieleza kwa ufasaha umuhimu wa upimaji na tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, asilimia 11.0 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani. Watahiniwa hao walitoa hoja chache kuliko zilizokuwa zinatakiwa na wengine walieleza baadhi ya hoja ambazo si sahihi kuhusu umuhimu wa upimaji na tathmini katika somo la Jiografia hivyo kupata alama pungufu. Kwa mfano, baadhi ya hoja ambazo siyo sahihi zilizoandikwa na watahiniwa ni pamoja na jinsi upimaji na tathmini vinavyosaidia katika kumotisha na kuandaa mafunzo ya walimu kazini, kuwapandisha walimu madaraja na kuwafanya wanafunzi kuwa na uhuru wa kujifunza zaidi.

Aidha, uchambuzi ulionesha asilimia 1.5 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu wenye alama 0 hadi 1.5. Wengi wa watahiniwa hawa, walieleza hoja tofauti na matakwa ya swali, ingawa hoja hizo zinahusiana

na upimaji na tathmini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *(i) ili tathmini itokee lazima upimaji uanze, (ii) kutumiwa yote kwa lengo la kufanya maboresho (iii) kutumiwa kwa zana za upimaji na tathmini katika majibu* na *(iv) yote hutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi maarifa aliyofundishwa.* Majibu haya ni dhahiri kuwa mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali, hoja yake (i) si kweli kwamba upimaji unaanza kabla ya tathmini. Kimsingi tathmini ni endelevu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji na hufanyika kabla, wakati na baada ya ufundishaji. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.



(a) Upimaji hufanyika baada ya mafunzo na kabla ya mafunzo
(b) Upimaji humhusisha mwalimu na mwanafunzi
(c) Tathmini hufanywa wakati wa ufundishaji na baada ya ufundishaji
(d) Tathmini hufanywa na mwalimu kila siku awapo darasani na baada ya kufundisha.

Kielelezo Na.4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali hili.

Katika kielelezo Na 4.2, mtahiniwa alieleza hoja mbalimbali ambazo hazibainishi umuhimu wa upimaji na tathimini katika somo la Jiografia. Aidha, hoja zake zimejikita kueleza wahusika wa upimaji na tathmini na wakati gani upimaji na tathmini vinafanyika. Kimsingi, hoja zake siyo sahihi na hii ni kiashiria kuwa mtahiniwa alikuwa na uelewa hafifu kuhusu umuhimu wa upimaji na tathmini.

### 2.1.5 Swali la 5: Nchi yetu Tanzania

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya Nchi yetu Tanzania. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kubainisha mbinu nne zinazoweza kutumika katika kukabiliana na changamoto za makazi katika mji ambao umegundulika kuwa na madini. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hilo ulikuwa mzuri kwa kuwa, asilimia 82.6 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 5.





**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 5*

Kama Chati Na. 5 inavyoonesha, asilimia 41.8 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4. Asilimia 40.8 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 17.4 ndio walio na ufaulu hafifu kwa kiwango cha alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa uliofanyika kwenye skripti zao ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri (41.8) walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya watu na makazi. Watahiniwa hao walieleza kwa ufasaha mbinu stahiki zinazoweza kutumika katika kukabiliana na changamoto za makazi katika sehemu kulikogundulika madini. Miongoni mwa masuluhisho yaliyotolewa na watahiniwa hao ni pamoja na kuanzishwa kwa makazi mapya yaliyopangwa, kupima maeneo na kusimamia ujenzi bora ili kuepusha majanga, na kutoa elimu ya mazingira ili kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Pia, watahiniwa hao walieleza kuanzishwa kwa miradi ya uzalishaji mali kwa ajili ya watu wasio na kazi kwa kutumia sayansi na teknolojia ili kupunguza vitendo vya uhalifu. Vilevile, walitoa hoja ya kuboresha huduma za jamii vijijini na mjini kama vile afya, elimu na umeme ili kupunguza watu kuhamia mjini kwenye madini toka vijijini. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu sahihi katika kundi hilo.


5
i/ Ujenzi wa Miundombinu bora katika miji tofauti tofauti
ii/ Upatikanaji wa huduma za Kijamii au Uwepo wa huduma za Kijamii katika miji yote
iii/ Uwepo wa ajira. Serikali iweze Kuajiri watu ili Kuzuia na mlundikano wa Watu Sehemu moja
iv/ Utoaji wa Elimu kwa Wananchi. yaani watu waelimishwe juu ya Changamoto zinazo weza Kutokea Kutokana na mlundikano wa Watu. Mfano: Magonjwa.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 5.


Jibu la mtahiniwa katika Kielelezo Na. 5.1, linaelezea mbinu zinazoweza kutumika kukabiliana na changamoto ya makazi katika eneo lililogundulika kuwa na madini.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani (40.8) waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele. Katika kundi hili, baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza ufumbuzi wa changamoto za makazi kwa hoja pungufu ya nne zilizotakiwa na wengine walirudia hoja ambazo wamekwishazieleza. Pia, wapo watahiniwa walitaja hoja bila ufafanuzi kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika, *(i) kuweka mipaka, (ii) kutoa elimu, (iii) kuunda sheria na kanuni* na *(iv) kupanga miji.* Majibu haya ni kiashiria tosha kuwa wengi wa watahiniwa katika kundi hili walikuwa na uelewa wa wastani kwenye mada iliyotahiniwa.

Kwa upande mwingine, asilimia (17.4) ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikuwa na uelewa hafifu wa mada ya watu na makazi. Watahiniwa hawa walieleza hoja tofauti na utatuzi wa changamoto za makazi. Wapo watahiniwa walioeleza athari za uchimbaji madini au kanuni bora za uchimbaji wa madini, badala utatuzi wa changamoto za makazi katika eneo la madini. Baadhi ya athari za uchimbaji wa madini zilizobainishwa na watahiniwa hao ni pamoja na; *mmonyoko wa udongo, kuenea kwa magonjwa kama vile kifua kikuu, ukataji ovyo wa miti* pamoja na *uharibifu wa mazingira kwa ujumla.* Aidha, baadhi ya watahiniwa katika kundi hii walieleza njia zifaazo kuchukuliwa na makampuni ya uchimbaji wa madini

ili kuboresha maisha ya wachimbaji kwa kuwaongezea mishahara na marupurupu.

Kwa ujumla, watahiniwa wengi katika kundi hili walishindwa kutofautisha changamoto za watu na makazi katika eneo la madini na changamoto cha uchimbaji madini. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi katika kundi hilo.


5

i) Mbinu ya amani kupata haki zao.

ii) Mbinu ya kutumia makubaliano.

iii) Mbinu ya kusainishana mikataba.

iv) Mbinu ya kushirikiana nao ili kupata makazi yao.


Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 5.

Kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alieleza mbinu za kutumika kuondoa migogoro kwa wachimbaji wa madini na sio ufumbuzi wa changamoto za makazi katika maeneo ya uchimbaji madini.

### 2.1.6 Swali la 6: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika

Swali la 6 lilitungwa kutoka katika mada ya Vitangilizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi kwa kutoa mafunzo manne ambayo Waafrika wanaweza kujifunza kutokana na kushindwa kwao kuzuia ujio wa wakoloni katika bara la Afrika japo chini ya viongozi mbalimbali walipinga uvamizi huo.

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa wa mzuri kwani asilimia 73.4 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 6*

Takwimu katika Chati Na. 6 zinaonesha kuwa asilimia 35.4 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 38.0 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 26.6 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri ambayo ni asilimia 35.4 yanaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mafunzo ambayo Waafrika wanaweza kujifunza kutokana na kushindwa kwao na uvamizi wa kikoloni. Hivyo, hoja zao zilijikita katika kueleza mafunzo mbalimbali kwa Waafrika. Watahiniwa walieleza kuwa matumizi ya zana bora na mbinu za kisasa katika jambo lolote yanaweza kuleta ushindi. Wakaongeza kuwa, wakati wa uvamizi jamii nyingi zilitumia zana duni ikilinganishwa na zana bora za wakoloni.

Pia, walieleza kuwa kila jambo linahitaji maandalizi bora na umakini ili kuleta mafanikio. Hapa walitoa hoja kuwa jamii nyingi za Kiafrika ziliingia vitani bila kufanya upembuzi yakinifu wa nguvu ya adui hivyo ziliingia vitani bila maandalizi ya kutosha. Aidha, walionesha kuwa ushirikiano unahitajika katika kuleta ushindi. Katika hoja hii, watahiniwa wengi walifafanua kuwa wakati wa uvamizi wa kikoloni, jamii nyingi za Kiafrika hazikuungana pamoja kuwakabili wakoloni bali kila jamii ilipigana peke yake. Watahiniwa waliongeza kuwa, usaliti na unafiki haufai. Hapa walieleza kuwa wakati wa vita dhidi ya uvamizi wa kikoloni, baadhi ya jamii za Kiafrika zilishirikiana wa wakoloni kuzipiga jamii nyingine za Kiafrika. Kielelezo Na. 6.1 kinavyoonesha jibu sahihi la mtahiniwa katika kundi hilo.


| | |
|---|---|
| 6 | Umoja ni nguvu Utengano ni udhaifu mojawapo |
| | ya mafunzo ni kwamba ukuwa na umoja ma |
| | wezo mtaganya jambo kubwa kwa sababu wa |
| | afrika hawakuwa na ushirikiano walishindwa. |
| | -Maandalizi bora ni Muhimu katika Vita. pia |
| | hapa kutokana na kwamba waafrika walikuw |
| | a na Maandalizi duni ndiyo Maana walishi |
| | ndwa kuwapiga Wakoloni. |
| | -Mbinu bora za Kivita ni Muhimu katika mapigano |
| | pia kutokana na kwamba Waafrika walikuwa na |
| | Mbinu duni za kivita ndiyo Maana walishindwa |
| | -Usaliti hautakiwi katika jamii: kwa sababu waa |
| | frika walikuwa wanasalitiana ndiyo Maana |
| | Walishindwa kuwapiga wakoloni badala yake |
| | walipigwa wao wenyewe. Hii yote ni sababu ya Usaliti. |

Kielelzo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 6.

Katika kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alieleza mafunzo manne ambayo Waafrika wanaweza kujifunza kutokana na kushindwa kwao wakati wa ujio wa wakoloni katika bara la Afrika kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani (38.0) katika swali hili walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walitoa hoja pungufu, na wengine walishindwa kutoa sababu zilizojitosheleza. Aidha, watahiniwa wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yao. Lakini pia, wapo baadhi ya watahiniwa walioorodhesha hoja pasipo kutoa maelezo yoyote. Kwa ujumla, hoja zilizotolewa na watahiniwa wengi katika kundi hili zinaashiria kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu uvamizi wa kikoloni katika Afrika.

Kwa upande mwingine, majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu (26.6) hawakuelewa mahitaji ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika madhara ya biashara ya utumwa, njia zilizotumika kuwakamata watumwa, sababu zilizowafanya wakoloni kuja Afrika, madhara ya ukoloni na uchumi wa kikoloni. Aidha, watahiniwa wengine walieleza malengo ya elimu ya kikoloni, malengo ya wakoloni katika kueneza dini, na changamoto zilizowapata Waafrika wakati wakipigania uhuru wao. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi la katika kundi hili.



6


i) Kuwa wanyengekevu kwa wakoloni.
Sababu wakoloni walianzia kodi
ambapo mwaafrika ilihitaji kufanya kazi
ili apate kipato alipe kodi.
ii) Walijifunza kufunga na kutibu vidonda.
Sababu waafrika wengi walikuwa hawana
elimu jibu ya kufunga na kutibu vidonda
iii) Walijifunza kujenga miundombinu.
Sababu kazi ngumu walipewa
waafrika wafanye hivyo ilisaidi wao
kujua kujenga reli, barabara na majengo.
iv) Alifanya migomo baridi.
Sababu waafrika walikuwa hawapendi
wakoloni walifanya migomo baridi ilivaondeke.

Kielelzo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alitoa hoja ambazo ni kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano hoja (ii) na (iii) zinaeleza shughuli walizofanya Waafrika wakati wa ukoloni, na sio mafunzo waliyopata kutokana na kushindwa kupinga ujio wa ukoloni.

### 2.1.7 Swali la 7: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika. Katika kujibu swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kutoa hoja nne za kupinga usemi wa kuwa "Wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara walikuwa Afrika ili kuleta ustarabu mpya na sio kwa maslahi ya kiuchumi". Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 77.2 walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 7*


Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ambapo, asilimia 59.9 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 17.3 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 22.8 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mahitaji ya swali. Hii ni kwa kuwa kwani waliweza kutoa hoja nne zinazopinga usemi wa kuwa "Wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara walikuwa Afrika ili kuleta ustarabu mpya na sio kwa maslahi ya kiuchumi". Watahiniwa katika kundi hilo, walitoa hoja kuwa wavumbuzi walijifunza mila na tamaduni za Kiafrika zilizowawezesha kufahamu nguvu na udhaifu wao, hivyo ikawa rahisi kuwatawala. Hapa, watahiniwa walieleza kuwa harakati za vitangulizi vya ukoloni katika kuhimiza matumizi ya lugha za kigeni, elimu ya kikoloni, kuchunguza ardhi yenye rutuba, kutafuta masoko na malighafi kulifanyika ili vitangulizi hivyo viweze kutimiza maslahi yao ya kiuchumi.

Kwa mfano, katika majibu yao, watahiniwa walieleza jinsi wavumbuzi walivyopeleleza nguvu za kijeshi na silaha walizonazo Waafrika, na kutoa taarifa kwa mataifa yao. Taarifa hizo ndizo zilizorahisisha uvamizi na ushindi wa majeshi yao dhidi ya majeshi ya jamii za Kiafrika. Vilevile, walieleza jinsi wamisionari walivyoeneza dini ya Kikristo kwa lengo la kulainisha mioyo ya Waafrika ili waweze kuukubali utawala wa Wazungu kama mpango wa Mungu. Aidha, watahiniwa hao walieleza jinsi wafanyabiashara walivyotia saini mikataba ya ulaghai ambayo baadaye

ilitumiwa na mataifa hayo kuhalalisha uvamizi dhidi ya jamii mbalimbali za Kiafrika.

Aidha, majibu ya aina hii ni kielelezo kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa ujio wa wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara katika bara la Afrika. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa mmojawapo katika kundi hilo.


7

(i) Wavumbuzi walikuja kw Afrika kwa lengo la kukagua hali ya hewa ya Afrika, pia kukagua ardhi iliyo na rutuba.

(ii) Wafanyabiashara walikuja Afrika kwa lengo la kupata mali ghafi kwa ajili ya kuendesha bidhaa zao.

(iii) Wamisionari walikuja kwa lengo la kueneza dini ya kikristo ambapo waliunda makanisa mfano: C.M.C (church misionary

(iv) Wafanyabiashara walikuja Afrika kwa lengo la kupata masoko Atakayoendesha bidhaa zao.

Kielelezo Na.7.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alielezea kwa usahihi kuwa kuja kwa wavumbuzi, wafanyabiashara na wamisionari katika bara la Afrika kabla ya ukoloni ilikuwa ni kwa ajili ya maslahi yao ya kiuchumi.

Kwa upande wa watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani (17.3), majibu yao yalionesha kuwa, walikuwa na upungufu wa maarifa katika ujio wa wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiasha barani Afrika. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliandika hoja sahihi pungufu, au walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Wengi wa watahiniwa katika kundi hili walishindwa kutofautisha majukumu ya vitangulizi vya ukoloni na wakoloni. Aidha, baadhi yao walihusisha shuguli kama kuwanyanganya Waafrika ardhi, kuwalazimisha Waafrika kulipa kodi, na kuwanyonya Waafrika kwa kuwalipa ujira kidogo. Uchambuzi unaonesha pia watahiniwa hao walirudia baadhi ya hoja kwa maneno tofauti kama hoja tofauti kitu kilichofanya wakose baadhi ya alama.

Katika swali hili, kulikuwa na watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu (22.8%). Sababu kubwa za watahiniwa hao kuwa na ufaulu hafifu ni kutoa hoja pungufu, na wengine kuandika majibu ambayo ni shughuli mbalimbali

walizokuwa wanafanya wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara ili kukamilisha malengo yao ya kuja Afrika. Kwa mfano, katika kujibu swali hilo, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yake kama ifuatavyo;

(i) *Walijenga miundombinu kama reli, barabara na meliambavyo viliwasaidia usafiri mbalimbali.*
(ii) *Walileta mfumo wa mpya wa utoaji elimu rasmi darasani ambapo wameenda kupata elimu darasani*
(iii) *Walileta mfumo mpya wa kiutawala mfano kutoka mfumo wa kitemi kwenda mfumo mpya*
(iv) *Walileta mazao mapya na tamaduni mpya kama uvaaji wa mavazi mbalimbali na mazao mapya ya chakula kuyaleta huku Afrika, hii imekuwa moja ya mabadiliko ambayo yamechukua nafasi kutokana kuja kwao. Mwisho wameleta mfumo wa ela kwa kununua.*

Majibu haya ya mtahiniwa yanaashiria kuwa hakuwa na maarifa mahsusi kuhusi ujio wa wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara kabla ya ukoloni. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili hawakuandika chochote, na wengine waliandika majibu ambayo yaliashiria hawakuelewa matakwa ya swali. Hivyo walitoa majibu ambayo hayakuendana na swali kama Kielelezo Na. 7.2 kinavyoonesha.


| | |
|---|---|
| 7 | si kweli kwa sababu zifuatazo |
| | i/ walikuja kufundisha ufugaji, kwa kufuga mifugo |
| | mbalimbali kwa njia |
| | mbalimbali |
| | ii/ walikuja kufundisha biashara mbalimbali, walileta bia |
| | shara ili kuweza kujiongezea pato na kuinua uchu |
| | mi wa nchi |
| | iii/ walikuja kufundisha kilimo, kwa kuonyesha mbi |
| | nu mbalimbali za kufanya kilimo ili kuzalisha |
| | mazao ya chakula na biashara |
| | iv/ walikuja kutoa elimu, ili kuweza kuwasaidi |
| | a waafrika katika biashara zao na wajue kuso |
| | ma, kuandika na kuhesabu. |

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 7.

Majibu ya mtahiniwa katika kilelelezo Na. 7.2 hayana uhusiano wowote na swali. Swali linataka kuonesha malengo ya kuja kwa wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara kabla ya ukoloni. Kwenye majibu ya mtahiniwa, hakuna jibu lolote linaloeleza malengo ya watu hao kabla ya ukoloni.

### 2.1.8 Swali la 8: Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Historia. Katika kujibu swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza mambo manne ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa zana za kufundishia mada ya mifumo ya uzalishaji mali katika zama za chuma. Kwa ujumla ufaulu katika swali hilo ulikuwa mzuri kutokana na asilimia 98.5 ya watahiniwa kupata alama 2 hadi 4, kama Chati Na. 8 inavyoonesha.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa swali la 8*

Takwimu katika Chati Na. 8 zinaonesha kuwa, watahiniwa asilimia 94.9 walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4. Watahiniwa wengine asilimia 3.6 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 1.5 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, asilimia 94.9 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walizingatia matakwa ya swali. Kwani wengi wao walieleza mambo muhimu ya kuzingatia kama vile uhusiano wa zana na mada inayofundishwa. Watahiniwa walieleza kuwa, uhusiano wa zana na mada hurahisisha ujifunzaji na kusaidia kueleweka kwa dhana ambazo zisingeeleweka bila zana. Watahiniwa hawa pia walieleza muonekano mzuri wa zana, na wengine wakafafanu kuwa uzuri wa zana; kwa maana ya ukubwa wa zana, kusomeka kwa maandishi au picha na mvuto wa zana. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *(i) kuandaa zana inayoendana na lengo mahususi la somo husika, (ii) kuandaa zana inayoendana na umri na uelewa wa wanafunzi, (iii) kuandaa zana*

*inayofikirisha na kukuza uwezo wa wanafunzi kudadisi* na *(iv) kuandaa zana inayovutia ili kuvuta usikivu wa wanafunzi husika.*

Vilevile watahiniwa walieleza kuwa zana inatakiwa iwe rahisi kueleweka ikiwa haina fumbo, hivyo kurahisisha ujifunzaji kwa wanafunzi. Katika kuonesha kuwa walilielewa swali, pia walieleza hoja ya kuwa zana ni lazima iwe rahisi kutunza bila gharama au gharama nafuu, na itumike kwa muda mrefu. Wengine waliongeza hoja ya kuwa lazima zana izingatie umri wa wanafunzi, na isiwe hatarishi kwa wanafunzi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja katika hoja yake ya nne aliandika; *zana itayoandaliwa lazima izingatie suala la kutoogopesha wanafunzi darasani*. Hoja hii inaeleza suala la kuzingatia umri na kutokuwa hatarishi darasani.

Mtahiniwa mwingine katika kujibu swali hilo alito hoja zifuatazo;


*(i)* *Zana lazima iendane na lengo mahususi, hii itafanya wanafunzi kuelewa juu ya kile kinafundishwa darasani,*

*(ii)* *Zana lazima ivutie kwa wanafunzi, hii itasaidia kuvuta umakini zaidi wa wanafunzi katika ujifunzaji,*

*(iii)* *Zana lazima ichochee udadisi kwa udadisi, hii itasaidia wafanye uchunguzi wa kina kwa kuuliza au kujibu maswali,*

*(iv)* *Zana lazima iwe yenye kuonekana vizuri darasani ili kila mwanafunzi aweze kuiona hiyo zana na iendane na ukubwa wa darasa.*

Majibu ya mlengo huu yameonekana katika watahiniwa wengi wenye ufaulu mzuri. Kilelelzo Na. 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa lililo sahihi katika kundi hilo.


8 (i) Zana inayoendana na lengo mahususi hivyo Basi zana inatakiwa kulengo uzalishaji kipindi cha zama za chumu

(ii) Zana iwe na uwezo wa kumufikiisha na kumudadisi Mwanafunzi ili kuweza kubaini kweli hiyo zana inaweza kutumika kwa uzalishaji mali zama za chuma

(iii) Zana iwe inaendana na umri wa walengwa. hivyo basi unatakiwa kuandaa zana ya kulikuna a umri wa wanafunzi wako darasani ambalo unafundisha


(iv) zana iwe na ukubwa unaofaa, ili kuweza kuonekana darasani pindi unapokuwa unafundisha

Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi kwa swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa katika majibu yake alieleza uandaaji wa zana unaozingatia uhusiano wa mada husika ambayo ni zama za chuma. Pia zana izingatie ukubwa unaofaa, yaani iweze kuonekana kwa wanafunzi wote. Kwa ujumla, hoja alizozieleza zinatosheleleza kusema kuwa ni majibu sahihi kwa swali la 8.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani (3.6%) umeonesha kuwa, watahiniwa hao walichanganya baadhi ya hoja zilizohusu uandaaji wa zana katika uzalishaji wakati zama za chuma na mbinu za kufundishia. Kwa mfano mtahiniwa aliandika; *(i) kuandaa mada ya kufundishia na kujifunzia (ii) kuendana na lengo au lengo mahususi (iii) kuchagua mbinu au njia za ufundishaji (iv) kuzingatia umri na uelewa wa walengwa pamoja na ukubwa wa darasa.* Katika majibu ya mtahiniwa, hoja ya kwanza na ya tatu zinaongelea mbinu za ufundishaji badala namna bora uandaaji za zana. Mchanganyiko huo wa hoja ulisababisha watahiniwa hao kupata alama za wastani kati ya 2 hadi 2.5, kati ya alama 4 za swali hilo.

Watahiniwa asilimia 1.5 waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuweza kutoa hoja sahihi kuhusu uandaaji wa zana za kufundishia katika mada ya uzalishaji wakati wa zama za chuma. Kwa mfano mtahiniwa aliandika; *(i) nitaandaa panga (ii) jembe (iii) mkuki (iv) shoka.* Watahiniwa hawa walielezea aina ya zana alizotumia binadamu wakati wa zama za mawe. Kilelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa.



| 8 | |
|---|---|
| (i) | Kuzingatia kiwango cha akili walichokuwa nacho watu wa kale cha kutengeneza vitaa walivyokuwa wanavitumia |
| (ii) | Kuzingatia muundo wa vyuma waliokuwa wakiutumia watu wa kale |
| (iii) | Kuzingatia aina za vifaa walivyokuwa wakivitumia watu wa kale |
| (iv) | Kuzingatia Ubora wa zana walizokuwa wakizitumia watu wa kale kufuatana na zama zote tatu za chuma. |


Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 8.

.

Katika kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa katika hoja zake alielezea uandaaji wa zana katika zama za mawe. Alionesha wale waaandaji walizingatia mambo gani katika kuziandaa zana hizo. Kwa ujumla, mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali.

### 2.1.9 Swali la 9: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru

Swali hili lilitungwa kutoka mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru. Katika kujibu swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi athari nne zinazotokana na migogoro ya kisiasa inayosababishwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe katika baadhi ya mataifa ya Kiafrika kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudani Kusini na Somalia. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, kwa ujumla, ufaulu katika swali hilo ulikuwa mzuri kwa kuwa, asilimia 95.4 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 9 inaonesha kwa muhtasari ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 9*

Kama Chati Na. 9 inavyoonesha, asilmia 92.5 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilmia 2.9 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2 hadi 2.5, na asilimia 4.6 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5, ambapo asilimia 2.9 kati yao walipata 0.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umebaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri (92.5%) walieleza kwa ufasaha athari za migogoro ya kisiasa katika nchi tajwa. Watahiniwa hao waliweza kubainisha kuwa migogoro husababisha mauaji ya watu wengi wasio na hatia kutokana na makundi yanayopigana kushambulia raia. Nia ya mashambulishi hayo ni kuidhalilisha serikali inayoongoza ili ionekane imeshindwa kuwalinda wananchi wake. Watahiniwa walieleza kudumaa kwa uchumi kunakosababishwa na watu kushindwa kufanya kazi wakihofia mapigano. Pia walieleza kuwa uharibifu mkubwa wa mali kama vile nyumba, majengo ya biashara, magari na miundombinu hutokea. Vita huongeza chuki na uhasama miongoni mwa wananchi kwa mtizamo wa ukabila, ukanda wa udini kama ilivyo nchini Nigeria, Sudani, Rwanda, Burundi na Uganda.

Uchambuzi pia umebaini kuwa watahiniwa walieleza migogoro kusababisha nchi hizo kuingiliwa na mataifa makubwa ambayo huwa sio tu kutuliza migogoro bali ni kulinda maslahi yao ya kiuchumi, kimkakati na kisiasa. Vilevile watahiniwa walibainisha kuwa migogoro husababiaha njaa kwani serikali na waasi huzuia misafara ya kupeleka chakula katika sehemu ambazo ni ngome za wapinzani wao; kwa mfano Sudani, Somalia na Ivory Coast. Mwisho, walieleza kuwa migogoro huzalisha wakimbizi wa kisiasa.

Kwa mfano, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zimezalisha wakimbizi wanaoishi katika nchi za Tanzania, Uganda na Zambia. Kielelezo Na. 9.1 ni mfano wa jibu sahihi la mtahiniwa mmojawapo katika hili kundi.

| 9 | |
|---|---|
| | (i) Vifo, migogo inaweza kusababisha vifo kwa watu kwani watapigana hatimaye kusababisha vifo kutokea ambayo itapunguza idadi ya watu katika nchi ambazo zina migogoro ya kisiasa. |
| | (ii) Kuporomoka kwa uchumi wa nchi, nchi zenye migogoro ya kisiasa zitashindwa katika kuendeleza uchumi wao kwani kutatokea kuharibiwa kwa miundombinu pia bidhaa zitashindwa kusafirishwa. |
| | (iii) Kuongezeka kwa idadi ya wakimbizi, migogoro pia inapelekea kuongezeka kwa idadi ya wakimbizi ambao watakimbilia nchi zingine ili kunusuru maisha yao. |
| | (iv) Utengano wa familia, migogoro pia inasababisha familia kutaweka na hivyo kutengana katika harakati za kunusuru maisha yao. |


Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa alitoa hoja nne za athari za migogoro ya kisiasa katika nchi za Kiafrika, ambazo zinajibu matakwa ya swali kwa usahihi.

Uchambuzi wa majibu ya asilimia 2.9 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani umeonesha kuwa, watahiniwa hao walieleza hoja zisizojitosheleza. Baadhi pia waliandika hoja kwa kurudia ambazo zilipelekea kupata alama pungufu. Wengine walieleza hoja zilizopelekea nchi kuwa na migogoro, badala ya athari za migogoro. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *hoja mojawapo kuwa kukithiri kwa rushwa kutokana na viongozi wengi kupenda vitendo vya ubadhilifu wa mali za umma*. Hoja hii inaeleza chanzo cha migogoro, na sio athari za migogoro. Mtahiniwa mwingine aliandika; *(i) kudumaza maendeleo ya kiuchumi; migogogoro inapotokea huweza kupelekea kutokuwa na maendeleo nchini (ii) kutokutekeleza matakwa ya wananchi; migogoro ya kisiasa inapojitokeza katika nchi hupekelea viongozi kushindwa kutekeleza matakwa ya wananchi (iii) sera mbovu; migogoro inaojitokeza katika nchi hupelekea viongozi kuwa na sera mbovu* na *(iv) vifo; migogogo inapojitokeza katika nchi huweza kupelekea vifo kutokea katika eneo.*

Katika majibu ya mtahiniwa hoja (ii) na (iii) kimsingi sio athari za migogoro bali ni sababu au vichocheo vya migogoro.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu (4.6%) walitoa hoja tofauti na matakwa ya swali. Watahiniwa hao walitoa hoja ambazo hazikuonesha athari zozote zilizotokana na migogogro. Watahiniwa wengine wa kundi hili walichanganya hoja zinazohusu sababu zinazoweza kuchangia migogoro kutokea kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *(i) uongozi mbaya (ii) kutokuwepo kwa demokrasia (iii) ukiukwaji na unyanyasi wa kijinsia (iv) tofauti ya serikali na dola za kiislamu au taasisi za dini*. Katika jibu hili mtahiniwa hakueleza kama tofauti za kidini zinajitokeza au ni chanzo cha migogro. Mtahiniwa mwingine aliandika kama ifuatavyo: *(i) uongozi mbaya ni chanzo cha migogoro hiyo unakuta serikali au nchi hiyo inaongozwa bila demokrasia. (ii) rushwa pia ni chanzo cha migogoro hiyo utakuta viongozi wanatumia pesa ovyo (iii) maisha magumu ni chanzo cha migororo hiyo kwani wananchi ni hali ngumu kupita kiasi wanashindwa kumudu* na *(iv) kutokuwa na mgawanyo wa madaraka ni sababu ya migogoro hiyo*. Majibu katika hoja (ii) na (iii) ni vyanzo vya migogoro, kinyume na swali lililohitaji athari za migogoro. Keielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa mmojawapo katika kundi hilo.



9
a) Tamaa za madaraka - hii ni kutokana na kila mtu kutamani kuongoza nchi au kuwa madarakani kwa manufaa yake binafsi
b) Dini - hii ni kutokana na baadhi ya watu kutaka watu wote waamini wanachokiamini wao
c) Ubaguzi - hii ni kutokana na jinsia moja kujiona bora kuliko jinsia ya tofauti hivyo kwa jinsia ya wanaume kubagua wanawake
d) Maelewano duni - Pia migogoro hii inatokea pale baadhi ya watu kutokuwa na maelewano baina ya wenyewe kwa wenyewe.

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2, majibu ya mtahiniwa yalikuwa na dosari, hivyo kupata alama hafifu. Kimsingi hoja zote nne zilieleza vyanzo vya migogoro, na sio athari za migogoro.

### 2.1.10 Swali la 10: Ushirikiano wa Kimataifa

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Ushirikiano wa Kimataifa. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi malengo manne ya kuundwa kwa umoja wa mataifa, baada ya vita ya pili ya Dunia. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo kwani asilimia 89.5 walipata alama kati ya 2 hadi 4, kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 10.





**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 10*

Takwimu katika Chati Na. 10 zinaonesha kuwa, asilimia 70.5 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 3 hadi 4, asilimia 19.0 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 2.0 hadi 2.5, na asilimia 10.5 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, ufaulu mzuri wa asilimia 70.5 ya watahiniwa ulitokana na watahiniwa hao kuweza kutoa hoja tatu hadi nne kwa usahihi. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Ushirikiano wa Kimataifa, na hasa kuundwa kwa Umoja wa Mataifa. Watahiniwa hao walieleza malengo mbalimbali ya kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa. Hoja zilizojitokeza zaidi kwa watahiniwa walio wengi ni pamoja na; *kudumisha amani, usalama na ushirikiano baina ya mataifa*; *kuendeleza mahusiano ya kirafiki baina ya nchi mbalimbali*; *kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinaheshimiwa kulingana na Mkataba wa Umoja wa Mtaifa wa 1948; kuwawezesha wanachama kushirikiana katika kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika nchi mbalimbali na kuweza kusaidia kutatua migogoro. Kwa mfano migogoro ya mipaka kati ya nchi na nchi, kama*

*mgogoro wa Ethiopia na Eritrea* pamoja na *kuboresha hali ya maisha ya watu wote Duniani hasa uwezo wa kupata mahitaji muhimu ya kibinadamu.* Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa mmojawapo katika kundi hilo.



10
i) kuliundwa umoja wa Mataifa ili kudumisha umoja na Mshikamano kwa nchi wanachama.
ii) kuliundwa umoja wa Mataifa ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi zote.
iii) kuliundwa umoja wa Mataifa ili kutetea haki za binadamu.
iv) kuliundwa Umoja wa Mataifa ili kusaidia kuboresha Maisha ya wananchi katika nchi wanachama.

Kielelezo Na.10.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.1, mtahiniwa aligusia baadhi ya malengo ya kuundwa kwa umoja wa mataifa. Hata hivyo, hoja yake ya nne siyo sahihi sana kwa kuwa lengo mojawapo lilikuwa ni kuboresha hali ya maisha ya watu wote Duniani, hasa uwezo wa kupata mahitaji muhimu ya kibidamu na sio kwa wanachama peke yao.

Uchambuzi zaidi ulioneshwa kuwa asilimia 19.0 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani baadhi yao waliweza kueleza hoja mbili kwa ufasaha na kueleza hoja nyingine mbili ambazo hazikuwa zinajibu swali kikamilifu. Pia, baadhi ya watahiniwa walieleza masuala ya kutetea Afrika kupata uhuru. Watahiniwa hao walichanganya dhana ya malengo ya Umoja wa Afrika au Afrika Mashariki na dhana ya malengo ya Umoja wa Mataifa. Aidha, baadhi ya watahiniwa walitoa hoja tofauti kama vile kukomesha biashara ya watumwa na unyanyasaji katika makoloni yao, hivyo kusababisha kupata alama hafifu. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *(i) kudai uhuru kwa nchi za Afrika kutoka kwa Wazungu, (ii) kuimarisha umoja na mshikamano kwa nchi mwanachama, (iii) kuimarisha ulinzi na usalama* na *(iv) kudumisha na kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa nchi mwanachama*. Majibu ya mtahiniwa kwa hoja (i) na (iv) sio malengo ya Umoja wa Mataifa, bali ni malengo ya Umoja wa Afrika Mashariki.

Watahiniwa asilimia 10.5 waliokuwa na ufaulu hafifu kwenye swali hilo walitoa majibu ambayo yalionesha kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu malengo ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa, na hivyo kuwafanya washindwe kutoa hoja zilizoendana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja zifuatazo; *(i) kupinga unyonywaji unaofanywa na wakoloni (ii) kupinga unyanyasaji dhidi ya watu weusi unoafanywa na wakoloni (iii) ili kudai uhuru wa Waafrika dhidi ya wakoloni* na *(iv) kujenga nguvu moja ya kupinga ukoloni*. Katika hoja zote nne za mtahiniwa, hakuna hoja hata moja ambayo inagusia Umoja wa Mataifa. Mtahiniwa huyo kwa ujumla alieleza malengo ya Umoja wa Afrika. Aidha, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili hawakuandika chochote, na wengine waliandika malengo ya Wakoloni kuja Afrika. Kielelezo Na. 10.2 kinaoonesha jibu la mtahiniwa lisilo sahihi.


10

(i) Kupeta viongozi bora.
Baada ya vita vya pili vya dunia kuliundwa kwa umoja wa mataifa ili kuweza kuungana na kupata viongozi bora

(ii) Kukomesha biashara ya utumwa
Lengo la kuundwa kwa umoja wa mataifa ni kukomesha biashara ya utumwa.

(iii) Kupuka unyanyasaji

(iv) Kuondoa ukabila baina ya mataifa.

Kielelezo Na.10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alitoa hoja ambazo ni kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, hoja (ii) ya kukomeshwa kwa biashara ya watumwa sio sahihi, biashara hiyo ilikomeshwa karne ya 19 kabla ya kuundwa kwa umoja wa mataifa.


## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Insha

Sehemu B katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali manne ya insha ambayo mtahiniwa alitakiwa kujibu yote. Maswali mawili ya taaluma; moja lilihusu somo la Jiografia na moja somo la Historia. Pia kulikuwa na maswali mawili ya ufundishaji na ujifunzaji; moja lilihusu somo la Jiografia na moja somo la Historia. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na uzito wa alama 15. Kwa ajili ya kufanya uchambuzi na tathmini, ufaulu wa watahiniwa katika kila swali uligawanywa katika

mkundi matatu; ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri. Mfiko wa alama katika kila kundi ulikuwa 0-5.5, 6-10.0 na 10.5-15 mtawalia.

### 2.2.1 Swali la 11: Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika

Swali hili lilitoka mada ya Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kuchambua shughuli tano kuu za kiuchumi zilizofanywa katika hatua mpya ya kuimarisha uchumi wa kikoloni, pamoja na kwamba jamii nyingi za Kiafrika zilipinga uvamizi huo. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo kwani asilimia 98.0 walipata alama kati ya 6 hadi 15 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 11*

Takwimu katika Chati Na. 11 zinaonesha kuwa, asilimia 53.9 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15, asilimia 44.1 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6.0 hadi 10.0, na asilimia 2.0 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0.0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri (53.9%) waliweza kuchambua kwa ufasaha shughuli za kiuchumi zilizoanzishwa na wakoloni barani Afrika. Shughuli ambazo watahiniwa wengi walizichambua ni pamoja na; kilimo cha mazao ya biashara, uchimbaji wa madini, uanzishwaji wa viwanda vilivyolenga kupunguza uzito malighafi, biashara za kuuza na kununua kwa kutumia pesa na ujenzi wa miundombinu ili kurahisha usafirishaji wa malighafi. Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha wa shughuli kuu za kiuchumi wakati wa ukoloni hivyo, waliweza

kutoa majibu yaliyokidhi mahitaji ya swali. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mmojawapo wa watahiniwa katika kundi hilo.


11 Uchumi wa kikoloni, ni shughuli zote za uzalishaji mali ....... zilizoanzishwa na wakoloni kwa lengo la kujiimarisha kiuchumi wao wenyewe na kuwanyonya waafrika katika karne ya 19. Wakoloni walianza kuja Afrika kwa lengo la kujiimarisha kiuchumi kwa sababu walona Afrika kuna malighafi kwa ajili ya viwanda vyao, ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo, wafanya-kazi na uzuri wa hali ya hewa.

Zifuatazo ni shughuli za kiuchumi zilizofanya katika hatua za kuimarisha uchumi mpya wa kikoloni:-

Kilimo, wakoloni walianzisha mashamba makubwa ya kilimo cha biashara na kuwakataza waafrika kulima mazao ya chakula. Walianzisha mashamba ya katani, pamba na karafuu kwa ajili ya viwanda vyao. Waliwafanyisha kazi waafrika muda mrefu na kuwalipa ujira mdogo.

Viwanda, walianzisha viwanda vidogo-vidogo kwa lengo la kuchakata malighafi na kuzifanya kuwa nyepesi na kuzipeleka huko Ulaya mfano viwanda vya uchakataji wa katani.

Uchimbaji wa madini, walianzisha migodi mbalimbali kwa ajili ya kupata madini na kuyapeleka kwao mfano Tanzanite, Almasi na dhahabu. Walitumia madini haya kutengeneza bidhaa mbalimbali na kuja kutuuzia


11 Cont. Biashara, wakoloni walianzisha biashara ya kubadilishana bidhaa kwa bidhaa hivyo wao waliwalichukua vitu vyetu vya thamani na kutupa vya kwao. Mfano, walibadilishana pembe za ndovu kwa cheni, madini kwa kioo, hivyo ilipelekea wao kujiimarisha kiuchumi zaidi.

Uchukuzi na usafirishaji, wakoloni waliboresha miundombinu kwa lengo la kurahisisha zoezi la kuchukua malighafi kutoka Afrika na kuzipeleka ulaya hali hii iliwafanya wao waweze kuimarisha uchumi wao.

Hivyo basi japokuwa waafrika walipinga uvamizi wa kikoloni walishindwa kutokana na ~~na~~ kukosa jeshi imara, pamoja na silaha za kivita hivyo waafrika waliendelea kunyonywa rasilimali zao Mfano madini, kupora ardhi yenye rutuba na pia kufanyishwa kazi kwa ujira mdogo hali hii ilipelekea wakoloni kujiimarisha kiuchumi zaidi.


Kielelezo Na.11.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.1, mtahiniwa alitoa hoja tano ambazo zilijibu matakwa ya swali kwa usahihi. Kwa mfano kilimo, viwanda, biashara, uchimbaji wa madini na uchukuzi ni shughuli kuu zilizofanywa na wakoloni kuimarisha uchumi wao.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, asilimia 44.1 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na dosari chache kwenye majibu yao. Baadhi yao waliandika hoja chache kuliko hoja zilizokuwa zinahitajika. Wengine waliandika kwa kurudia hoja, hivyo kupata alama pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kuwa, shughuli kuu za kiuchumi zilizoanzishwa na wakoloni ni; *(i) kuanzishwa kwa kilimo kama pamba, mahindi, maharage, karanga na karafuu (ii)shughuli za ufugaji wa kondoo, mbuzi, ngombe nk (iii) uchimbaji wa madini (iv) shughuli za uvuvi* na *(v) kuanzishwa kwa viwanda*. Majibu ya mtahiniwa katika hoja (i) (ii) na (iv) yote yapo katika hoja moja ya kilimo na mifugo. Watahiniwa wengine waliandika hoja ambazo hazikuwa na mantiki, au hazikukidhi mahitaji ya swali. Kwa mfano mtahiniwa aliandika hoja mojawapo kuwa; *kuanzishwa kwa dini ya Kikristo iliyoenezwa na wamisionari*. Hapo inaonesha mtahiniwa amechanganya shughuli

zilianzishwa wa watangulizi wa ukoloni na wakati wa ulokoni. Hivyo majibu hayo yamepelekea kupata alama pungufu.

Watahiniwa wachache (2.0%) waliokuwa na ufaulu hafifu katika swali hili walieleza shughuli ambazo hazikuwa sahihi kulingana na mahitaji ya swali. Shughuli zilizoelezwa ni uanzishwaji wa biashara ya watumwa, kulipa kodi, kuanzisha masoko ya bidhaa zao, biashara ya utalii, kuimarisha sekta ya elimu na afya, na kutafuta vibarua nafuu. Jibu la kulipa kodi halikuwa shughuli ambayo ilianzishwa ili kuimarisha uchumi wa kikoloni, bali ilianzishwa ili kuwafanya Waafrika wafanye kazi katika mashamba, viwanda au ujenzi wa miundombinu kwa ujira kidogo. Na walioshindwa kulipa kodi walilazimsihwa kufanya kazi kwenye mashamba ya wakoloni kufidia kodi ambayo hawakulipa. Majibu kama hayo yalifanya watahiniwa kupata alama hafifu kutokana na kuchanganya shughuli za vitangulizi vya ukoloni na shughuli nyingine ambazo zilikuwa ni matokeo ya shughuli mama za kiuchumi. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi.


11

Shughuli za kiuchumi ni vitendo vinavyofanywa na jamii katika kupata mahitaji yote ya msingi. Kuna nyanja mbalimbali za uchumi mfano nyanya ya utalii, uadini na kilimo. Zifuatazo ni shughuli za kiuchumi

Shughuli ya uzalishaji mali. Wavamizi wa kikoloni waliimarisha sekta mbalimbali mfano sekta ya madini, kilimo ili kuweza kuzalisha bidhaa ili kuweza kupeleka katika nchi zao.

Shughuli ya utoaji huduma. Pia iliimarisha sekta ya Afya ili kuweza kupata huduma kwa jamii na kuepuka kupoteza maliasili watu kwa ukosefu wa huduma za jamii.

shughuli ya usambazaji. Pia palikuwa na shughuli ya usambazaji wa bidhaa kupitia nyanja ya usafirishaji na mawasiliano. Waliimarisha sekta hizi ili waweze kusambaza bidhaa zao.

Shughuli za uwekezaji. Uchumi wa kikoloni ulitegemea sana shughuli za uwekezaji Afrika ambapo ilipelekea nyanja ya biashara kuendelea kwasababu wakoloni waliwekeza sana katika nchi za Afrika. Katika nyanja zote za kiuchumi.

Shughuli za ukusanyaji kodi. Pia wakoloni walianzisha kodi kwa ajili ya maslahi yao kiuchumi. Walikuwa wanakusanya kodi walikuwa na kodi ya kichwa na kodi ya mafuta.

Kwahiyo, wakoloni walikuwa na shughuli za uzalishaji mali, utoaji huduma, usambazaji, uwekezaji na ukusanyaji kodi kwa waafrika


Kielelezo Na.11.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2, hoja za mtahiniwa nyingi zinahusu mambo yaliyojitokeza katika kuimarisha shughuli za kiuchumi za kikoloni. Shughuli mama za kuimarisha uchumi wa kikoloni alizitaja kama mifano ya uzalishaji mali. Hitaji la swali lilikuwa kueleza uanzishwaji wa kilimo na uanzishwaji wa viwanda. Aidha, shughuli zilizobainishwa na mtahiniwa ni muhimu wakati tayari shughuli mama zimekwishaanzishwa.

### 2.2.2 Swali la 12: Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo

Swali la 12 lilitungwa kutoka mada ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja tano kueleza namna ya kutatua changamoto ya uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la

Historia katika shule za sekondari. Uhaba huo husababisha ugumu wa ufundishaji na ujifunzaji. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo kwani asilimia 89.58 walipata alama kati ya 6 hadi 15 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** Ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 12

Chati Na. 12 inaonesha kuwa, asilimia 57.1 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 14.5, asilimia 35.5 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10, na asilimia 10.4 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa, asilimia 57.1 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kutoa hoja ambazo zilieleza njia tano anazoweza kutumia mwalimu katika kutatua changamoto ya zana za kufundishia somo la Historia kama vile; *kutengeneza; ambapo mwalimu anaweza kupata zana kwa kuchora, kuumba, kufinyanga au kukata na kubandika,, kununua;mwalimu anaweza kununua zana mbalimbali kutoka katika maduka ya vifaa kama Taasisi ya Elimu Tanzania, maduka ya vitabu, maonesho ya vitabu na viwanda uchapishaji. Kuazima ambapo mwalimu anaweza kupata zana kutoka kwa mwalimu mwingine, au taasisi mbalimbali za kielimu zilizo jirani. Kufaranga ambapo mwalimu anaamua kubuni kifaa kingine mbadala wa kifaa husika pale kifaa halisi kinapokuwa hakipatikani. Kukodi ambapo mwalimu hutumia gharama ili kupata kifaa anachohitaji. Kuokota; mwalimu hukusanya vitu mbalimbali kwa kufanya ziara katika mazingira halisi. Kusoma taarifa mbalimbali kama matini, vitabu, magazeti na majarida katika maktaba na mitandao ya intaneti.*

Majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa walikuwa wana uwezo wa kubainisha namna ya kutatua changamoto za zana za kufundisha na kujifunzia. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa.

12 Zana za kufundishia na kujifunzia ni nyenzo
ambazo husaidia na kurahisisha suala nzima
la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la historia.
Zana za kufundishia na kujifunzia huwa katika
makundi ya masikizi, zana maono na zana masikizi
maono, ambapo katika somo la historia zana maono
huweza kuwa ni picha, chati na michoro, zana
masikizi huweza kuwa redio, simu, kanda za kaseti,
zana masikizi huweza kuwa televisheni zote hizo
hurahisisha suala zima la ufundishaji na ujifunzaji.
Njia ambazo mwalimu anaweza kuzitumia
katika kutatua changamoto ya uhaba wa zana
za kufundishia na kujifunzia ni kama zifuatazo;
Njia ya kutengeneza; mwalimu wa somo la
historia anaweza kutatua changamoto ya uhaba
wa zana za kufundishia na kujifunzia kwa-
kutumia njia ya kutengeneza zana mbalimbali
kwa kutumia malighafi mbalimbali zinazopatikana
katika mazingira anayoyaishi na mazingira mengine.
Njia ya kutengeneza mwalimu anatakiwa kutenge-
neza zana hiyo hatua kwa hatua kwa muda mrefu
kidogo. Mfano mwalimu anaweza kutengeneza zana
kama mti wa familia kwa kutumia vibao vya miti.
Njia ya kufaragua; mwalimu anaweza
kuondoa uhaba wa zana kwa kufaragua zana kwa
kutumia makunzi mbalimbali yanayopatikana katika
mazingira aliyopo kwa muda huo kwasababu kufara-
gua haihitaji kutumia muda mwingi ili kupata zana
kwa kuiga mfano wa kitu halisi papo kwa papo.
Njia ya kufaragua ni njia nzuri kwasababu haitumii
muda mwingi kuandaa zana hizo kwaajili ya
kufundishia na kujifunzia somo la historia.

12 Cont.

Njia ya kuazima; mwalimu wa somo la historia anaweza kuondoa uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia kwa kuazima zana mbalimbali za kufundishia kutoka shule ambazo ni za jirani ambazo huweza kutunza zana za kufundishia na kujifunzia au kuazima maktaba ambazo ni za umilliki wa watu au zinamilikiwa na serikali yenyewe. Mfano mwalimu anaweza kuazima michoro, picha na chati mbalimbali ili aweze kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la historia.

Njia ya kukusanya na kuokota; pia mwalimu anaweza kupata zana kwa njia ya kukusanya na kuokota vitu mbalimbali ambavyo vinaendana na maudhui ya somo analotaka kufundisha ili kumrahisishia katika suala nzima la ufundishaji na ujifunzaji ili wanafunzi waweze kuelewa somo kwa urahisi na kwa haraka zaidi, pia ili kuwajengea kumbukumbu ya muda mrefu. Mfano wa zana ni kama kuokota mifupa, au vifaa vya kutumika katika uzalishaji mali kama jembe, mundu, panga.

Njia ya kununua, njia ya kununua mara nyingi huwa ni ya mwisho endapo mwalimu na mwanafunzi watashindwa kutengeneza, pia watashindwa kufaragua, kuazima, kuokota na kukusanya mwalimu ndipo huchukua maamuzi ya kwenda kununua zana mbalimbali ambazo zinaendana na kufundishia na kujifunzia somo la ~~jiograf~~ historia. Njia ya kununua hutumia gharama, haikuzi kipaji cha mwanafunzi kwasababu mwanafunzi hawezi kushinki katika utengenezaji. Zana zinazonunuliwa ni kama vile picha mbalimbali za viongozi mashujaa wa kiafrika Mfano J.K Nyerere.

12 Cont.

Hivyobasi, tunapaswa kutatua changamoto ya uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la historia kwasababu zana zikitumika darasani wakati wa kufundishia na kujifunzia humsaidia mwanafunzi kuelewa somo kwa urahisi, kulipenda na kufurahia somo, kukuza udadisi wa mwanafunzi humsaidia mwalimu kuwa na maneno machache wakati wa ufundishaji na ujifunzaji kwasababu zana ni zaidi ya maneno elfu ya mwalimu.

Kielelezo Na.12.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 12.

Katika kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa alitoa hoja tano zinazoonesha namna ya kutatua changamoto ya zana za ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Historia kwa usahihi.

Katika swali hili, asilimia 32.5 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani. Uchambuzi wa majibu ulibaini kuwa watahiniwa hao walikuwa wanaeleza njia moja katika hoja mbalimbali wakidhani ni njia tofauti. Kwa mfano mtahiniwa alieleza kuchonga, kuchora na kufuma kama njia tatu tofauti wakati njia hizi zinafafanua zaidi njia moja ya kutengeneza. Uchambuzi umebaini kuwa sababu za watahiniwa kushindwa kueleza njia sahihi ilitokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya kutengeneza zana. Katika kutengeneza zana, mwalimu anaweza kuchora, kuumba, kufinyanga, kukata na kubandika au kuchonga. Kushindwa kwa watahiniwa kutambua aina za utengenezaji wa zana kwenye hoja zao uliosababisha watahiniwa hao kupata alama za wastani (6 – 10).


Kwa upande mwingine, asilimia 10.2 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikuwa na changamoto ya kutofautisha njia za kupata zana na mbinu za kufundishia. Pamoja na kwamba watahiniwa walitakiwa kueleza njia zinazotumika kutatua changamoto ya uhaba wa zana, watahiniwa katika kundi hilo walichanganya mbinu za kufundishia na kujifunzia na njia za kutatua uhaba wa zana katika kufundisha na kujifunzia somo la Historia. Kwa Mfano mtahiniwa mmoja alieleza hoja hizi; *majadiliano, kumualika mgeni, onesho mbinu, ziara na kazi mradi.* Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walitoa hoja ambazo zilielezea namna ya kuhifadhi zana za ufundishaji na ujifunzaji, hivyo kuwafanya wapate alama hafifu. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *kuhifadhi zana kwenye kabati, kutundika zana kwenye ukuta* na *kuhifadhi zana kwenye chumba maalum.* Majibu haya hayakuwa sahihi kwa sababu kuhifadhi zana siyo namna ya kutatua changamoto ya uhaba wa zana ingawa inasadia. Ni kweli kuwa kuhifadhi zana kunaweza kusaidia upatikanaji wa zana, lakini si sahihi kwa sababu zinazohifadhiwa ni zile zilizo haba hivyo hazitatosheleleza kwa mahitaji husika. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya jibu hafifu kutoka kwa mmojawapo wa watahiniwa katika kundi hili.

Uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la historia bado ni tatizo linalojitokeza katika baadhi ya shule za msingi. na hivyo kusababisha ugumu katika. ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anaweza kutatua changamoto hizo kwa kufanya. mambo mbadala wa zana za kufundishia na kujifunzia kama ifuatavyo.

Kufanya ziara mara kwa mara. mwalimu wa somo la historia katika. kutatua changamoto ya uhaba wa zana anapaswa kufanya ziara mara kwa mara na wanafunzi wake kwenda maeneo. ya kihistoria na majumba ya makumbusho kujifunza kwa vitendo zaidi kuliko. nadharia.

Vitabu vya ziada na machapisho mbalimbali:- mwalimu wa somo la. historia kutokana na uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia ili aweze. kutatua changamoto hii katika ufundishaji na ujifunzaji anapaswa kuandaa vitabu vya ziada na machapisho mbalimbali yanayohusiana na matukio ya kihistoria.

Kitabu cha ziada ni kitabu. kinachotoa ufafanuzi zaidi ya yale yaliyoko kwenye muhtasari wa somo la historia. kitabu hiki mwalimu na mwanafunzi wana weza kutumia katika ufundishaji na. ujifunzaji ili kuweza kutatua changamoto za uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia


12 Cont.

kitabu cha mwanafunzi:- hiki ni kitabu ambacho mwanafunzi hutumia. ambacho huwa na maelezo ya umahiri mkuu na mahususi. kitabu hiki cha mwanafunzi huwa na picha zinazoonesha kumbukumbu za matukio ya kihistoria. hivyo itakuwa ni moja ya mbinu ya kutatua changamoto ya zana za kufundishia na kujifunzia.

Mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji: mwalimu wa somo la historia ili aweze kutatua changamoto ya uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzi anaweza aka tafuta mtandaoni namna matukio yalivyo fanyika mfano vita ya kwanza ya dunia na vita ya pili ya dunia na kisha kuwaonesha wanafunzi video hizo kupitia Sinema.


Hivyo basi uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la historia ni changamoto kwa baadhi ya shule za msingi ningependa kuwa shauri walimu na chama cha walimu. kuomba serikali iwasaidie namna ya kukabiliana na uhaba huo wa zana. Pia walimu wanaweza kutumia mbinu hizi kutatua changamoto hiyo ya uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia.

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.2, mtahiniwa alitoa hoja ambazo ni kinyume na matakwa ya swali. Hoja zote zilieleza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, badala ya njia ya kupata zana za ufundishaji.

### 2.2.3 Swali la 13: Dunia Sayari

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Dunia Sayari. Katika swali hilo, mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja tano kuthibitisha kuwa Dunia ni duara. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo kwani asilimia 92.7 walipata alama kati ya 6 hadi 15, kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 13.




**Chati Na. 13**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 13*


Takwimu katika Chati Na 13 zinaoonesha kuwa asilimia 31.0 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15, asilimia 61.7 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10, na asilimia 7.3 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri (31.0%) umeonesha kuwa, watahiniwa hao waliweza kueleza hoja zinazothibitisha kuwa Dunia ni duara. Watahiniwa hao walitoa hoja kama vile, utofauti wa kutokea kwa mawio na machweo katika Dunia, kuzunguka Dunia kwa meli ambapo mwisho kurudi pale ilipoanzia, picha za satellite kuonesha Dunia ina umbo la mviringo, kuonekana kwa meli ikiwa mbali ambapo huanza kuonekana sehemu ya juu. Watahiniwa pia walieleza kupatwa kwa Mwezi ambapo Dunia inakuwa katikati ya Jua na Mwezi. Kwenye kitendo hiki, kivuli cha Dunia huonekana kwenye mwezi kikiwa na umbile la mviringo. Pamoja na kubadilika kwa umbali kati ya Jua na Dunia ambapo asubuhi na jioni Jua huonekana lipo karibu na Dunia, lakini mchana huonekana lipo mbali na Dunia. Pia watahiniwa walieleza uchunguzi wa kinajimu kuwa sayari zote na vitu vyote vina umbile la mviringo tufe, yaani si duara hasa. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa sahihi katika kundi hilo.

13 Dunia ni Sayari lililopo angani ambapo hulizunguka jua. Katika mpangilio wa Sayari dunia ni Sayari ya tatu ambayo ni Sayari pekee yenye uwepo wa viumbe hai na visivyo hai kuishi na kufanya Shughuli zao za kila siku. Dunia inasaidia maisha kuendelea kutokana na uwepo wa maji ya kutosha, nishati ya jua, nguvu ya uvutano inasababisha mjongeo wa viumbe hai na visivyo hai, hewa na msawazo mzuri yaani baridi kiasi na joto kiasi. Pia dunia ina mizunguko miwili ambayo ni dunia kujizungusha yenye kwenye mhimili wake kwa saa 24 (siku moja) na dunia kulizunguka jua siku 365 (mwaka mmoja). Zifuatazo ni hoja ambazo zinathibitisha kuwa dunia ni duara.

Picha za angani. Hii huonesha kwamba dunia ni duara na siyo tambarare wala umbo dufu, kwa sababu picha zote zinazochukuliwa kutoka angani huwa ni za duara. Hivyo huu ndio uthibitisho kwamba dunia ni duara, kwani picha zinge kuwa zinaonesha maumbo mengine mbalimbali basi tungesema kuwa dunia siyo umbo la duara, mfano picha za ramani ya nchi.

Kupatwa kwa mwezi. Hutokea pale ambapo dunia inakuwa kati ya jua na mwezi ambapo dunia huzuia mionzi au mwanga wa jua kufikia mwezi na kusababisha nuru ya mwezi kufifia na kuwa giza. Hivyo kivuli cha dunia ambacho huwa kinatua kwenye mwezi huwa na umbo la duara, hivyo huthibitisha kwamba dunia ni duara. Kama isingekuwa ni duara basi kivuli cha dunia kingeonekana na umbo lingine.



13 Cont.

Safari ya kuizunguka dunia. Katika
Safari ya kuizunguka dunia kwa njia ya miguu au
kwa kutumia vyombo vya usafiri huthibitisha kuwa
dunia ni duara, kwa sababu unapoanzia safari
ndipo hapo utakapo ishia yaani utazunguka lakini
hatimaye kurudi ulipoanzia, na kama ingekuwa duni
a ni tambarare basi tungekuwa tunaendelea kwenda
mbele bila kurudi tulipoanzia safari.
Mawio na machweo. Hii ina maana ya
Kuchomoza na kuzama kwa jua. Hii huthibitisha
kwamba dunia ni duara kwa sababu wakati wa
asubuhi jua huchomoza mashariki na kutua upande
wa magharibi hii hutokea kwa sababu dunia
hujizungusha kutoka magharibi kwenda mashariki, pia
kama dunia isingekuwa duara basi wakati wa asubuhi
sehemu zote za dunia zingekuwa zinaona jua kwa wak-
ati mmoja na kuona giza wakati mmoja kwahiyo
upande wa mashariki huona jua mapema kuliko
upande wa magharibi.
Kutofautiana kwa vipindi vya jua.
Wakati wa asubuhi na jioni jua huonekana lipo karibu
sana na uso wa dunia lakini wakati wa ~~wa~~
mchana jua huwa mbali sana dunia, hivyo hii
huthibitisha kwamba dunia ni duara.
Kwahiyo basi; Dunia inapofanya mizun-
guko yake miwili ya kujizungusha yenyewe
katika mhimili wake, na kulizunguka jua tunapa-
ta usiku na mchana, kupwa na kujaa kwa
maji, kutofautiana kwa urefu wa usiku na mchana
na majira ya mwaka ambayo ni kiangazi,
masika, kipupwe na vuli.

Kielelezo.Na. 13.1 Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 13.

Katika kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa alitoa hoja tano zinazothibitisha kuwa Dunia ni duara kwa usahihi.

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa asilimia 61.7 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu uthibitisho wa kuwa Dunia ni duara. Watahiniwa katika kundi hili walitoa uthibitisho wa; *kupatwa kwa Jua, kujaa na kupwa* na *umbali kutoka usawa wa bahari*. Katika hoja ya kupatwa kwa Jua, watahiniwa wameshindwa kutofautisha matukio ya wakati wa kupatwa kwa Mwezi na kupatwa kwa

jua. Kupatwa kwa Jua kunatokea wakati Mwezi unapita kati ya jua na Dunia hivyo kusababisha mwanga kupungua Duniani au giza kwa muda fulani. Hapo jua, Mwezi na Dunia vinakuwa katika mstari mmoja. Wakati kupatwa kwa Mwezi hutokea wakati Dunia inakuwa katikati ya jua na Mwezi, na kivuli cha Dunia huonekana katika Mwezi kikiwa cha mviringo. Baadhi ya watahiniwa pia walieleza kuwa Dunia ni mviringo kutokana na uthibitisho wa; *kupatwa kwa Dunia*. Hoja hii inathibitisha kuwa watahiniwa walioandika jibu hili hawana maarifa na mada ya Dunia Sayari, kwani hakuna hoja ya kupatwa kwa Dunia.

Watahiniwa wachache (7.3%) waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuelewa mahitaji ya swali. Hilo lilidhihirishwa kwa watahiniwa hao kuandika majibu yaliyokuwa na maelezo ya kina, lakini yasiyohusu mada ndogo ya mizunguko ya Dunia iliyokuwa inatakiwa kujibiwa. Watahiniwa katika kundi hili wapo ambao hawakujibu chochote na wengine walieleza umuhimu wa sayari Dunia kwa viumbe hai kama kielelezo Na. 13.2 kinavyoonesha.

**13**

Dunia, ni sayari ambayo viumbe hai
huishi, dunia ndiyo sayari pekee yenye -
uhai ambapo binadamu na viumbe hai
wengine huweza kuishi kwa kupata hewa
ya oksijeni na kuweza kutoa hewa ya -
kabondayoksaidi ambapo sayari nyingine
hazina sifa kama ya dunia. Zifuatazo ni
hoja zinazothibitisha kuwa dunia ni duara.

Dunia kujizungusha kwenye mhimili
wake; dunia inavyojizungusha kwenye -
mhimili wake tunapata mawio na
machweo ambapo huweza kujidhihirisha
kuwa dunia ni duara.

Dunia kulizunguka jua, Dunia kuli
zunguka jua tunapata majira ya mwaka
ambapo kuna vuli, masika, kipupwe -
na kiangazi, ambapo hii yote husababi
sha na dunia kuwa ya duara.

Kuwepo kwa mstari wa Ikweta;
mstari huu pia huweza kuonyesha kuwa
dunia ni duara kwa sababu mstari
huu huwa una nyuzi 0° ambapo -
husababisha kugawa dunia katikati

Majira ya mwaka, Tunapopata
majira ya mwaka huweza kusababishwa
na dunia kulizunguka jua na hivyo
kuweza kuthibitisha kuwa dunia ni
duara kwa sababu ya kujizungusha
katika mhimili wake.

Mawio na machweo, tunapothibi
tisha kuwa dunia ni duara tunaweza -
kuona dunia ikijizungusha katika mhimili

**13 Cont.**

wake tunaweza kupata mawio na machweo


Hivyo basi; Dunia ni duara kwa saba-
bu dunia inavyojizungusha kwenye mhimili
wake tunaweza kupata usiku na mchana
pia mawio na machweo pia dunia -
kulizunguka jua tunapata Majira ya mwaka.

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 13.

Katika Kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alielezea hoja ambazo hazithibitishi kuwa Dunia ni duara, badala yake zinaeleza tabianchi tofauti. Kimsingi, mtahiniwa alishindwa kufafanua kuwa Dunia kuzunguka Jua kunasabaisha kutokea kwa mawio na machweo kwa wakati tofauti katika Dunia, hivyo Dunia ni duara. Alieleza; *majira ya mwaka kiangazi na masika* na *kuwepo kwa mstari wa Ikweta* kama uthibitisho wa kuwa Dunia ni duara wakati hoja hii sio sahihi.

### 2.2.4 Swali la 14: Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo. Katika swali hilo, watahiniwa walitakiwa kueleza kwa ufasaha mambo matano ya kuzingatiwa na mwalimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia kwa njia ya majadiliano ya vikundi. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hilo, kwani asilimia 99.1 walipata alama kati ya 6 hadi 15 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Swali la 14*

Takwimu katika Chati Na 14 zinaoonesha kuwa asilimia 46.0 ya watahiniwa waliofanya swali hilo walikuwa na ufaulu mzuri wa alama 10.5 hadi 15, asilimia 53.1 walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10, na asilimia 0.9 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa, asilimia 46.0 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walieleza kwa ufasaha mambo matano ya kuzingatia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia kwa

kutumia njia ya majadiliano ya vikundi. Watahiniwa walieleza hoja kama vile; *kuongoza wanafunzi katika uundaji wa vikundi vinavyozingatia uwezo na uelewa na jinsi zote kwa idadi isiyozidi watu sita. Kuchagua viongozi wao yaani mwenyekiti, katibu na mtunza muda wa vikundi ambao watakuwa na jukumu la kuendesha na kusimamia mijadala katika vikundi. Mwalimu kutoa maelezo kuhusu muda wa kuwasilisha kazi zao zilizotokana na mijadala kwenye vikundi.* Watahiniwa wa kundi hili pia walieleza kuwa; *mwalimu anatakiwa kuhimiza kila mwanafunzi kuchangia mawazo na kuheshimu mawazo ya wengine na asiruhusu mmoja au wachache kutawala mjadala wakati wa majadiliano. Mwalimu apitie vikundi wakati wa majadiliano ili kusaidia au kutoa maelekezo ya kitu gani kifanyike katika vikundi au kuwauliza maswali wanafunzi yatayowafanya wafikirie zaidi katika kupata majibu ya kinachotakiwa.* Vilevile, watahiniwa walieleza kuwa; *wakati wa uwasilishaji wa majibu mwalimu asiruhusu kikundi kurudia majibu yaliyokwishawasilishwa na kikundi kingine ili kuepuka upotevu wa muda usio kuwa na sababu.* Majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa walikuwa na uwezo wa kueleza kwa ufasaha mambo ya kuzingatiwa na mwalimu wakati kufundisha njia ya majadiliano ya vikundi. Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa.

14 Njia ya majadiliano ni njia inayohusisha uundaji wa makundi na kujadiliana juu ya jambo fulani. Njia hii husaidia katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la jiografia kwa sababu husaidia mwalimu kubainisha changamoto za wanafunzi, pia husaidia mwalimu kubaini haiba za wanafunzi.

Yafuatayo ni mambo matano ya kuzingatia pale mwalimu anapotumia njia hii darasani ni kama ifuatavyo.

Uzingatiaji wa uwiano wa kijinsia hutokana pale mwalimu anapotumia njia hii azingatie uwiano wa kijinsia kwa kuunda makundi yenye idadi sawa ya jinsi za wanafunzi mfano kama kundi litakuwa na wanafunzi kumi basi wanafunzi watano ni wa kiume na watano wa kike.

Uundaji wa makundi, pale mwalimu anapotumia njia hii basi azingatie uundaji wa makundi kwani atatoa kazi zitakazojadiliwa na kuwasilishwa, mfano mwalimu aunde makundi yake ambayo yatajadili kazi yoyote aliotoa darasani.

Uzingatiaji wa kuteua uongozi wa makundi, hawa ni uongozi wanafunzi wenye jukumu la kusimamia na kuendesha kazi zote za kundi mfano kuteua mkuu wa kundi na katibu wa kundi ambao watasimamia na kuendesha majadiliano.

Kufatilia kazi za makundi katika majadiliano, pale mwalimu anapotembelea makundi itasaidia kuona kama kazi iliyotolewa

14 Cont. yafanyika au hapana. mfano kufatilia kama
wanajadiliana kwa ufasaha wala sio kufanya
kazi zao.
Kubakiwisha mawasilisho, yanafanyika, baa
da ya mwalimu kutoa kazi kwa makundi. lazim
a aruhusu wanafunzi wawasilishe kile walichojad
iliano ili kufanya maboresho na kubaini dosari
zilizopo, tokeza kwenye uwasilishaji huo.
Kuandaa kazi za makundi, hizi ni kazi
ambazo zinaandaliwa na mwalimu ili zitumi
ke katika makundi ya majadiliano katika somo
la jiografia. mfano kazi za makundi ni
maswali au maswali juu ya jambo fulani.
Hitimisho, licha ya njia ya majadilian
o kuwa na mambo ya kuzingatia pale inapo
tumika darasani lakini ya umuhimu au
faida kwa mwalimu au mwanafunzi kama hum
saidia mwalimu kubaini haiba na tabia za
wanafunzi pia hudumisha ushirikiano baina
ya wanafunzi na kujenga stadi za uongozi kwa
mwanafunzi

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 14.

Katika kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alitoa hoja zilizojibu matakwa ya swali, ingawa hoja ya kwanza ilikuwa na upungufu kidogo wa kutoonesha kuzingatiwa kwa uwezo na uelewa wa wana kikundi.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani (53.1%) walikuwa na mchanganyiko wa hoja zinazoelezea mambo ya kuzingatiwa na mwalimu wakati kutumia njia ya majadiliano ya vikundi, pamoja na mambo ya kuzingatiwa na mwalimu wakati wote wa ufundishaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa; *kuthibiti kelele na fujo darasani* na *kujadili kwa kutumia zana za mada inayofundishwa*. Mtahiniwa mwingine aliandika kuwa; *hali za wanafunzi kuzingatiwa kama familia duni, bora na zenye migogoro* na *wanfunzi wenye mahitaji maalum.* Hoja zote hizi zinazingatiwa wakati wote wa ufundishaji na sio maalum kwa njia ya majadiliano. Majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uwezo wa kupambanua bayana mambo muhimu ya kuzingatiwa na mwalimu wakati wa ufundishaji kwa njia ya majadiliano, na njia zingine za ufundiashaji. Watahiniwa hao waliyaona mambo hayo kama yanafanana.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu (0.9%) walibainika kutokuwa na maarifa juu njia ya majadiliano katika ufundishaji na ujifunzaji. Katika kundi hilo, baadhi ya watahiniwa walielezea mambo ya jumla ya kuzingatiwa katika ufundishaji kama vile mahitaji maalum wa uwepo wa zana. Kwa mfano, katika kujibu swali hilo, mtahiniwa mmoja aliandika mambo ya jumla ambayo ni; *umri wa walengwa, aina ya zana, mkao wa wanafunzi darasani, mahitaji maalum.* Mtahiniwa mwingine alieleza hoja za faida ya njia majadiliano kama *kutumika kuweka kumbukumbu kwa wanafunzi, kuchochea udadisi wa mwanafunzi, kuchochea ari ya kijifunza, mwanafunzi kujiamini* na *kuchochea ari ya kulipenda somo.* Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kuwa watahiniwa hao, hawakuwa na ufahamu juu njia ya majadiliano, hivyo kuwa na ufaulu hafifu kwenye swali hilo. Kielelzo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu la lisilo sahihi katika swali la 14.


[illegible]
njia (mbinu) mojawapo ya kutumia Mwalimu katika ufundishaji wake ili kuweza kufikisha ujumbe uliokusudiwa na kuweza kuelewa wanafunzi na kuwa wabunifu wa jambo fulani; yafuatayo ni mambo ya kuzingatia na Mwalimu wakati wa matumizi ya njia hiyo ya Majadiliano ya Vikundi darasani:-

Hutumika kuweka kumbukumbu kwa wanafunzi; Hii inamsaidia Mwanafunzi kukumbuka kile alichofundishwa na Mwalimu wake na kuweza kufikia kufahamu na kile alichokuwa anajadili kwenye Vikundi.

Kuchochea Udadisi; Hii ni njia mojawapo ya kujadili kwenye Vikundi. Mwanafunzi anakuwa anataka kujua kwa undani zaidi jambo fulani na kuweza kulifanyia kazi uchunguzi wa hali ya juu. Hivyo basi njia ya Majadiliano ya Vikundi ni mojawapo ya kumfanya Mwanafunzi kuwa Mdadisi wa jambo fulani.

Kuchochea ari ya kujifunza: Hii ni njia mojawapo ya kuwaweka wanafunzi kwenye Majadiliano ya vikundi ili waweze kujifunza kwa ufasaha na kuweza kuibua vipaji mbalimbali na kuweza kukuza Vipaji mbalimbali.

Mwanafunzi kujiamini: Hii inamsaidia Mwanafunzi pindi yuko pale anajadili na wenzake na kupata nafasi ya kuwasilisha taarifa mbele ya darasa -


14 Cont. na kuwa jasiri wa kusoma [illegible]
wengine na wenzake na kumuon-
dolea woga wa kuwa jasiri kila kiagizwa
Kuchochea ari ya kulipenda somo
Hii inatokea pale Mwanafunzi Anakuwa na
ari ya kufanya kazi kila Mara kwa Mara na
wenzake inamfanya kulipenda somo lake
la jiografia. Hivyo Mwalimu anahimizwa -
kuwahamasisha Wanafunzi wake katika vitu
vi mbalimbali.
Hivyo basi Njia ya Majadiliano ya
vikundi ni njia moja wapo inayo wezesha
ya wanafunzi kuongeza maarifa mbalimba
li na kujua vipaji mbalimbali.

Kielelezo Na.14.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alitoa hoja ambazo hazikukidhi matakwa ya swali. Kwa ujumla, hoja zote zilieleza umuhimu wa upimaji na tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, hoja ya kwanza hutumika kuweka kumbukumbu za wanafunzi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali za mtihani wa Maarifa ya Jamii ulikuwa mzuri. Mada zilizotahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii zilikuwa saba (7) ambapo mada sita (6) zilikuwa na ufaulu mzuri. Mada hizo ni: *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika* (98.1%), *Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo* (96.4%), *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru* (95.5%), *Ushirikiano wa Kimataifa* (89.5%), *Sayari Dunia* (81.7%), *Vitangulizi Vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika* (75.3%). Mada moja (1) ya *Nchi yetu Tanzania* ilikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 62.6.

Uchambuzi zaidi ulifanyika ili kubaini mwenendo wa ufaulu katika mada hizo kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2020. Uchambuzi huo umebaini kuwa, ufaulu umeendelea kuwa mzuri katika mada tano; *Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo* na *Ushirikiano wa Kimataifa.* Aidha mada za *Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika (64.9%), Sayari Dunia (62.9%), Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika (53.8%),* na *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika*

*Afrika Huru (49.0%),* zilikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia katika mwaka 2021, zimepanda hadi kiwango cha ufaulu mzuri cha asilimia mtawalia katika mwaka 2022. Kwa upande mwingine, ufaulu katika mada ya *Nchi yetu Tanzania* uliokuwa mzuri (88.4%) katika mwaka 2021 ila umeshuka hadi ufaulu wa wastani (62.6%) katika mwaka 2022.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchambuzi wa taarifa hii umeonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ni mzuri ikilinganishwa na ufaulu katika mwaka 2021, ufaulu umepanda katika baadhi ya mada. Uchambuzi umeonesha ongezeko la mada zenye ufaulu mzuri kutoka tano mwaka 2021 mpaka mada sita katika mwaka 2022. Katika mwaka 2022 hapakuwa na mada yenye ufaulu hafifu ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo kulikuwa na mada moja yenye ufaulu hafifu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua ufaulu katika mada ya Nchi yetu Tanzania, ambao ulikuwa wa kiwango cha wastani kutokana na kushuka kutoka ufaulu mzuri, yafuatayo yanapendekezwa kufanyika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Katika kuimarisha ufaulu katika mada ya Nchi yetu Tanzania;

(a) Walimu tarajali watumie mazingira halisi ikiwemo njia ya ziara ili kujifunza vipengele muhimu vya umbali katika Dunia kwa kutofautisha longitudo na latitudo, mwinuko kutoka usawa wa bahari, mikondo ya bahari na umbali wa eneo kutoka usawa wa bahari.

(b) Wakufunzi watumie mbinu shirikishi ili kuwawezesha walimu tarajali kuhusianisha vipengele muhimu vya umbali katika Dunia, na tabianchi tofauti wakitumia tufe na ramani, kwani hoja hii imeonekana kuwa tatizo kwa watahiniwa wengi.

(c) Walimu tarajali wapewe kazi mradi kuhusu tabianchi na hali ya hewa ili kuwajengea uelewa wa hali ya hewa na namna kila kipengele cha hali hewa kinavyoweza kuwa na tabianchi tofauti.

**KIAMBATISHO**

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MTIAHNI WA MAARIFA YAJAMII

| Na | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Watahiniwa waliopata wastani wa 40% ya alama au zaidi | Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika | 11 | 98 | 98 | Vizuri |
| 2. | Ufundishaji wa somo | 4 | 98.5 | 96.4 | Vizuri |
| | | 8 | 98.5 | | |
| | | 12 | 89.6 | | |
| | | 14 | 99.1 | | |
| 3. | Mabadiliko ya Kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru | 9 | 95.5 | 95.4 | Vizuri |
| 4. | Ushirikiano wa Kimataifa | 10 | 89.5 | 89.5 | Vizuri |
| 5. | Sayari Dunia | 3 | 82.6 | 81.7 | Vizuri |
| | | 13 | 70.3 | | |
| 6. | Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika | 6 | 73.4 | 75.3 | Vizuri |
| | | 7 | 77.2 | | |
| 7. | Nchi Yetu Tanzania | 1 | 17.2 | 62.6 | Wastani |
| | | 2 | 87.9 | | |
| | | 5 | 82.6 | | |